# Nipashe

Ijumaa Agosti 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580322

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Mbaroni tuhuma za kuwaua hawara, mtoto kisa mapenzi

UKURASA 5




UKURASA 11

# Kada wa CCM adaiwa kuuawa kwenye vurugu

• **Yadaiwa** zilihusisha wafuasi wa vyama vya siasa, watatu wajeruhiwa, polisi watoa tamko zito...*Endelea ukurasa 2*



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas (kulia), akiwa na Kamanda wa Mkoa wa Songwe, George Kiando (kushoto kwake) na maofisa wengine, wakikagua Ofisi ya Mtendaji Kata ya Mwaka Kati, yanapodaiwa kutokea mauaji ya mtu mmoja katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma, mkoani Songwe. **PICHA: JESHI LA POLISI**


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**TCRA YAIFUNGIA CLOUDS SIKU SABA**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), imesitisha utoaji wa huduma za...

UKURASA WA 4

**KIGOGO TRA KIZIMBANI MADAI KUKUSANYA KODI BILA UTARATIBU**

OFISA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Humphrey Lauwo, ame...

UKURASA WA 19

**MGOMBEA UDIWANI CCM AFARIKI DUNIA**

ALIYEKUWA Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Iringa, Onesmo...


## Wagombea zaidi urais wachukua fomu ZNZ

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store




## CHADEMA yalia wagombea 57 ubunge, 600 udiwani kukatwa

UKURASA 2

**MICHEZO** YACOUBA APEPERUKA, CARLINHOS ATOA NENO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kada wa CCM adaiwa kuuawa kwenye vurugu

**Na Thobias Mwanakatwe**

MTU mmoja amefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa ambao wanadaiwa kuwa ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya kutokea vurugu za kisiasa katika mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, akizungumza jana alimtaja aliyeuawa kuwa ni Braiton Mollel.

Waliojeruhiwa katika vurugu hizo zilizotokea kati ya wafuasi wa CCM na Chama cha Demokrsia na Maendeleo (CHADEMA) kuwa ni Elisha Mwaniemba, Fransis Simumba na Mtendaji wa Kata ya Mwaka Kati ambaye alidai jina lake halijapatikana.

Majeruhi Mwaniemba hali ni mbaya na amelazwa katika Hospitali ya Rufani Mbeya.

Kamanda Kyando alisema kufuatia tukio hilo watu 14, wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa wamekamatwa kwa tuhuma za mauaji ya kada huyo wa CCM.

Naye Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, ambaye yupo mkoani Songwe kwa ziara, ameagiza kukamatwa wote waliohusika iwe kwa kutamka, kupanga au kutenda katika tukio la mauaji ya Mollel.

Mollel aliyekuwa katika kitengo cha vijana wanaosaidia viongozi na Itifaki (UV-CCM), aliuawa kwa kushambuliwa na kundi la vijana waliovamia Ofisi za Mtendaji wa Kata ya Mwaka Kati Mjini Tunduma wakipinga kuenguliwa kwa mgombea wao baada ya kukosa sifa kugombea udiwani wa kata hiyo.

Alisema licha ya tukio hilo kufanywa katika mazingira ya kisiasa, lakini ni tukio la kihalifu.

Kamishna Sabas alivitaka vyama vya siasa nchini kuhakikisha vinafuata taratibu na miongozo iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ikiwamo kuheshimu sheria.

"Kabla ya kampeni kuanza NEC ilikutana na viongozi wote wa vyama vya siasa na kupewa taratibu...hivyo naomba kuwakumbusha wafuate taratibu hizo kinyume na hapo tutaendelea kuchukua hatua kali bila kujali nafasi ya mtu au chama anachotoka," alisema.

UV-CCM Mkoa wa Songwe imelaani tukio hilo, huku ikishusha lawama kwa Jeshi la Polisi Wilaya ya Momba kwa kushindwa kushughulikia taarifa za siri wanazopatiwa kuhusu vitendo vya uhalifu, likiwamo tukio hilo.

Mwenyekiti wa UV-CCM Mkoa wa Songwe, Andrew Kadeghe, alisema kabla ya tukio hilo kutokea CCM ilitoa taarifa ya maandishi kwa jeshi hilo kituo cha Tunduma juu ya njama na hujuma dhidi ya chama hicho.




Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia (CHADEMA), Benson Kigaila, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mwenendo wa wagombea wa chama hicho. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CHADEMA yalia wagombea wao ubunge 57 kuenguliwa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimedai wagombea wake 57 wa nafasi za ubunge na 600 wa udiwani wameshaenguliwa, kikiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua stahiki.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Tanzania Bara, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, aliitaka NEC kuwafuta kazi wasimamizi wa uchaguzi katika baadhi ya majimbo na kata zilizoonekana kuwa na kikwazo hicho na kuwarejesha wagombea wao walioenguliwa.

Benson Kigaila alisema kuwa iwapo tume haitafanya hivyo, chama hicho kitatangaza msimamo wao na kuongeza kuwa ni muhimu kwa tume kulinda haki za wagombea wote bila upendeleo.

"Kuna majimbo ambayo amechukua fomu mtu ambaye sisi hatumjui, tume ihakikishe majimbo hayo wagombea wetu wanapewa fomu, wanajaza na wanateuliwa kugombea," Kigaila alisema.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa CHADEMA, baadhi ya sababu za kuenguliwa kwa wagombea wao ni kutorudisha fomu za maadili, kutokuweka picha, wadhamini wa mgombea kutokuwapo kwenye orodha ya daftari la mpigakura, majina ya mgombea katika kitambulisho chake kutofautiana na majina katika fomu aliyojaza, Kigaila akidai kuwa ni za kusingiziwa.

Aliyataja majimbo na wagombea wao walioenguliwa kuwa ni pamoja na Butiama walilomteua Malato Marwa, Norbet Marandu (Handeni), Abubakari Mashambo (Bumbuli), Liberatus Lukurazo (Buhigwe), Msuka William (Mlele) na Stephen Hamis (Kavuu).

Wengine wanaodaiwa kuenguliwa ni Aisha Madoga (Dodoma Mjini), Essa Ngobei (Kongwa), Devotha Minja (Morogoro Mjini), Suzan Kiwanga (Mlimba), Hamad Kamtande (Liwale), Zamda Ngonyani (Namtumbo), Wolfgang Mwashambwa (Songwe), Fanuel Mkisi (Vwawa), Iddi Kizota (Kondoa Mjini), Bosco Mfundo (Gairo) na Khadija Omary (Kwimba).

Juzi, NEC kupitia kwa mkurugenzi wake, Dk. Wilson Mahera, ilitoa ufafanua kuhusu dosari zilizojitokeza katika mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ikiwamo ya kuenguliwa kwa baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani.

Dk. Mahera alisema tume inafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu hivyo hakuna mgombea atakayekatwa kwa matakwa fulani.

"Kuna taarifa mitandaoni watu wakilalamika kukatwa, suala la uteuzi mtu hawezi kukatwa kwa matakwa ya mtu. Tume inafanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni.

"Tumeweka kabisa sifa za wagombea katika ngazi zote za madiwani, wabunge na rais. Tumeweka pia masharti ya uteuzi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mbunge na diwani," alisema.

Dk. Mahera alisema kuwa kama mtu hajateuliwa, hajatekeleza masharti na kama mtu akitumia sababu nje ya hayo masharti hatafanikiwa.

"Huyo akikata rufani atashindwa. Tume inafanya kazi kuhakikisha kwamba shughuli zake zinafanyika kwa uwazi na uhuru na ukiangalia katika maelekezo ya wasimamizi wa uchaguzi, maelekezo kwa wasimamizi wa vituo vya kupiga kura, kwa vyama vya siasa na wagombea, yanaelekeza vizuri na yapo tovuti ya tume.

"Ukiona mtu anasema amekatwa, sijui hajateuliwa... maana yake ni vizuri uulize kwa msimamizi wa uchaguzi, akuelezee sababu ni nini, kwa mwenyewe ambaye hakupata uteuzi au upate ufafanuzi tume.

"Na sisi tume tupo tayari kushirikiana na ninyi ili uchaguzi huu uwe huru na haki, anayeshinda atangazwe, lakini tabia ya watu kuingia kwenye uchaguzi na hata kabla uchaguzi haujafanyika, tayari anajiona ni mshindi, hiyo ni tabia mbaya," alionya.

Dk. Mahera alisema sheria, kanuni na taratibu zitatumika kuhakikisha aliyeshinda ndiyo anapewa haki hiyo.

**HABARI KITAIFA**

# Wagombea Zanzibar wachukua fomu ZEC, watoa ahadi kemkem

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib (kulia), akipokea fomu ya kuomba uteuzi wa kugombea nafasi hiyo, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, mjini Zanzibar jana.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha NLD, Mfaume Khamis Hassan, akipokea fomu ya kuomba uteuzi wa kugombea nafasi hiyo, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, mjini Zanzibar jana.

WAGOMBEA watatu wa urais Zanzibar, jana walichukua fomu Tume ya Uchaguzi (ZEC) kugombea nafasi hiyo kupitia vyama vyao.

Kwa kuchukua kwao fomu, wamefanya idadi ya wagombea waliokwishafika tume kwa ajili hiyo kufikia watano hadi sasa, huku wengine wakitarajiwa kuchukua leo.

Waliojitokeza kwa siku ya jana ni Juma Ali Khatib wa Chama cha ADA-TADEA, aliyefika ZEC saa 4:00 asubuhi, Mfaume Khamis wa National League for Democracy (NLD) saa 5: 00 asubuhi na Hamad Rashid Muhamed wa ADC aliyefika saa 6:00 mchana.

Wagombea hao waliungana na Dk. Hussein Mwinyi wa Chama Cha Mapinduzi na Said Soud wa AAFP waliojitokeza juzi na kuchukua fomu kwa ajili ya kuomba kuteuliwa na ZEC kugombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu, Khatib alisema endapo atapata ridhaa ya kuwa Rais, atasimamia na kuendeleza miradi mikubwa ya maendeleo ambayo imeanzishwa na Raia anayemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein, ikiwamo ujenzi wa bandari, uwanja wa ndege Pemba na nyumba za makazi.

Pia alisema ataunda serikali ya umoja wa kitaifa kwa mujibu wa sheria na kuvishirikisha vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi mkuu.

Alisema kaulimbiu ya chama chake ni usawa kwa jamii na kwamba iwapo atachaguliwa, wananchi wote watapata huduma za kijamii zikiwamo elimu na afya.

Aidha, alisema endapo atashindwa katika uchaguzi mkuu yuko tayari kukubali matokea na kumuunga mkono aliyeshinda, huku akiwataka wagombea wenzake wa nafasi hiyo kutoka vyama vyengine, kufanya kampeni za kistaarabu ili nchi iendelee kuwa na amani wakati wote.

Naye Mfaume wa NLD alisema endapo atapata ridhaa, miongoni mwa vipaumbele vyake ni vijana kuwatumia katika harakati za maendeleo na kuwapatia ajira.

Pia alisema atahakikisha amani na utulivu inaimarika kwa sababu hakuna mbadala wa amani.

Hamad kwa upande wake alisema atahakikisha anasimamia haki ili wananchi wapate fursa mbalimbali zikiwamo za kiuchumi.

Alisema hivi sasa nchi iko katika uchumi wa kati, lakini wananchi hawajatambua uchumi huo, hivyo ADC itabadilisha taswira na kupata fursa wanazozihitaji na kwamba atahakikisha wananchi wanapata elimu kuanzia maandalizi hadi chuo kikuu bila malipo ili kuwa na wataalamu mbalimbali.

Sambamba na hilo, alisema atahakikisha anawalipa mishahara walimu wa madrasa kama ilivyo kwa walimu wa shule na kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa maji safi na salama.

Kabla ya kukabidhiwa fomu hizo, Mwenyekiti wa ZEC, Jaji mstaafu Hamid Mahamoud, aliwataka wagombea hao kufuata na kuheshimu kanuni na maadili ya uchaguzi za mwaka 2020 na kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

Alisema ni wajibu kwa wachukuaji fomu hizo kuzingatia muda wa kurejesha uliowekwa na tume ambao ni Septemba 9, mwaka huu, kabla ya saa 10:00 jioni wakiwa wametimiza masharti na vigezo.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADC, Hamad Rashid Muhamed, akipokea fomu ya kuomba uteuzi wa kugombea nafasi hiyo, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, mjini Zanzibar jana. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMA**

# Clouds yafungiwa siku saba

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), imesitisha utoaji wa huduma za utangazaji za Clouds FM na Clouds TV kwa muda wa siku saba kuanzia leo hadi Septemba 3, mwaka huu, kutokana na kukiuka kanuni za utangazaji na kanuni ndogo za utangazaji wa masuala ya uchaguzi za mwaka 2015.

Pia, ilivitaka vituo hivyo kuahirisha vipindi vyake vya jana na kuitumia siku hiyo kuomba radhi kwa Watanzania kwa kukiuka kanuni hizo.

TCRA imesema iwapo vituo hivyo vitashindwa, kukataa na kukaidi uamuzi huo, hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti zitachukuliwa dhidi yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa TCRA, James Kilaba, alisema kuwa Julai 10, 2010 na Julai 14, 2016, mamlaka hiyo ilivipa leseni vituo hivyo ya kutoa maudhui ya utangazaji.

Kilaba alisema kuwa Agosti 26 mwaka huu, kati ya saa 01:09 na saa 4:00 asubuhi, kupitia vipindi vya Clouds 360 na cha Power Breakfast, vilirusha takwimu za wagombea wa ubunge waliopita bila kupingwa huku taarifa hiyo ikiwa haijathibitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kukosa mizania.

"Kifungu cha 16(1) cha Kanuni za Utangazaji (Maudhui) na Kanuni Ndogo za Utangazaji wakati wa uchaguzi mwaka 2015 zinabainisha wajibu wa mtoa maudhui kutoa taarifa za matokeo ya uchaguzi kwa kadri zinavyopatikana na kutolewa na NEC na kuhakikisha matokeo yanatangazwa kwa ufasaha," alisema Kilaba.

Alifafanua kuwa kifungu cha 16(2) cha Kanuni za utangazaji wakati wa uchaguzi mwaka 2015, zinakataza mtoa huduma kutangaza maoni yatakayohamasisha vurugu au kuchochea chuki za kisiasa zinazoweza kusababisha madhara.

Alisema kifungu cha 5(j) cha kanuni za utangazaji wa kanuni ndogo za utangazaji wa masuala ya uchaguzi, kinamtaka mtoa huduma kufuata maelekezo yanayotolewa na sheria ya uchaguzi ambapo pamoja na mambo mengine mtoa huduma atatangaza matokeo kama yatakayotolewa na tume.

Kilaba alivitaka vyombo vya utangazaji kuzingatia kanuni hizo ili ziwawezeshe kutangaza masuala ya uchaguzi kwa weledi na kudumisha amani ya nchi.

# Saa 6 za pingamizi la Tundu Lissu NEC

**Na Mwandishi wetu,**

**DODOMA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), juzi ilitumia takribani saa sita kusikiliza mapingamizi yaliyowekwa na mgombea urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, dhidi ya wagombea wenzake wawili.

Juzi jioni, Lissu alifika kwenye ofisi za NEC na kuweka mapingamizi dhidi ya wagombea wenzake wawili, akidai wamekiuka sheria ya uchaguzi kifungu namba 38(4)(b).

Wagombea waliokuwa wamewekewa pingamizi ni Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli na wa Chama cha Wananchi(CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, ambao waliwasilisha utetezi wao tume.

Uchambuzi huo ulioanza majira ya saa 11 jioni, ulihitimishwa saa tano usiku juzi na tume ilitangaza uamuzi wa kutupilia mbali mapingamizi hayo baada ya kubaini hayana msingi wa kisheria.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, alisema kuwa Agosti 26 mwaka huu, tume ilipokea mapingamizi kutoka kwa Lissu dhidi ya Rais Magufuli na Profesa Lipumba.

Alisema kuwa kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 39(5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, wabunge za mwaka 2020, baada ya kupokea mapingamizi, tume iliwataarifu wahusika na kuwasilisha utetezi wao.

Alisema pingamizi dhidi ya Rais Magufuli lilikuwa kwamba hakuambatanisha picha kwenye fomu ya uteuzi na hakurudisha fomu ya uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria.

"Tume baada ya kupitia sababu za mapingamizi yote mawili pamoja na utetezi uliotolewa, imejiridhisha kuwa Magufuli amerejesha fomu zake ambazo zimeambatanishwa pamoja na picha kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo ya tume," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema tume imejiridhisha mapingamizi hayo hayana msingi wa kisheria na imetupilia mbali, hivyo Rais Magufuli ataendelea kuwa mgombea halali wa kiti hicho.

Kuhusu Profesa Lipumba, Dk. Charles alisema pingamizi lilikuwa hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa kisheria.

"Kwa mujibu wa kanuni ya 36(6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na wabunge mwaka 2020, sababu za uamuzi huu wa tume watapewa kwa maandishi aliyeweka na wale waliowekewa pingamizi, hivyo vyama vitakavyoshiriki uchaguzi vimebaki kuwa 15," alisema.

# Lissu atinga polisi kudai gari lake

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA), Tundu Lissu, jana alifika kwenye Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma kuomba kuchukua gari lake ambalo limehifadhiwa na Jeshi la Polisi Mkoa huo tangu lilipotokea tukio la kushambuliwa kwake kwa kupigwa risasi Septemba 7, 2017.

Vilevile, Lissu ambaye kitaalamu ni mwanasheria, alisema yuko tayari kuhojiwa na jeshi hilo kuhusu tukio hilo lililosababisha akae nje ya nchi kwa matibabu ya kibingwa kwa takribani miaka mitatu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na CHADEMA kwa vyombo vya habari jana, Lissu alifika kwenye ofisi hiyo akiwa amefuatana na mgombea mwenza wake, Salum Mwalimu na alipokewa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, Giles Muroto.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa katika mazungumzo yake na Kamanda Muroto, Lissu alisema ameamua kwenda mwenyewe baada ya utaratibu wa kulipata gari hilo kwa kuagiza watu wengine kushindikana.

Katika taarifa ya chama hicho, ilielezwa kuwa Kamanda Muroto alimweleza Lissu kwamba Jeshi la Polisi mkoani humo linahitaji muda zaidi ili kujiandaa kulikabidhi gari hilo kwake.

"Muroto alimweleza Lissu kwamba Jeshi la Polisi linamhitaji atoe maelezo kwa jeshi hilo kuhusu kushambuliwa kwake Septemba 2017.

"Lissu alijibu kwamba yuko tayari kutoa maelezo polisi kwa tarehe na muda utakaokuwa mwafaka kwa pande zote mbili.

Lissu alisema anashangaa kwamba hadi sasa, tangu kushambuliwa kwake miaka mitatu tangu iliyopita, Jeshi la Polisi halijafanya uchunguzi wowote, ikiwamo kumhoji yeye na dereva wake, Adam Bakari Mohamed," taarifa hiyo ya CHADEMA ilibainisha.

Alipoulizwa kuhusu suala hilo jana, Kamanda Muroto alisema Lissu alifika kwao kama wanavyofanya raia wengine wanapokuwa na shida za kuwasilishwa kwa Jeshi la Polisi.

Septemba 7, 2017, Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana akiwa kwenye gari lake nyumbani kwake mjini Dodoma, muda mfupi baada ya kumalizika kwa kikao cha mchana cha Bunge ambacho pia alichangia hoja akiwa Mbunge wa Singida Mashariki (CHADEMA).



Wajasiriamali wakiendelea na utengenezaji wa vyombo vya kulishia kuku kwa ajili ya kuuza ili kujipatia riziki, katika Soko la Temeke Vetenari jijini Dar es Salaam jana. **PCHA: JUMANNE JUMA**

# Kigogo TRA kizimbani madai kukusanya kodi bila utaratibu

**Na Hellen Mwango**

OFISA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Humphrey Lauwo, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na shtaka la kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1. 8 za kodi bila kufuata utaratibu.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shahidi. Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simoni alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Julai 2, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Ilidaiwa kwamba, mshtakiwa akiwa Ofisa Forodha Mwandamizi wa TRA, alikusanya Sh. 1,803,323,055 bila kuruhusiwa na TRA.

Ilidaiwa alikusanya fedha hizo ambazo zilitakiwa zilipwe kama kodi na Kampuni ya Puma Energy Tanzania Limited.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo. Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Mshtakiwa huyo alirudishwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ambayo ni kuwa na wadhamini wawili wenye vitambulisho watakaotia saini bondi ya Sh. milioni 40 kila mmoja.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 9, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

## Profesa Kabudi awashukuru Kilosa

**Na Mary Geofrey,** KILOSA

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, amewashukuru wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kumdhamini kuwania ubunge wa Kilosa.

Alitoa shukrani hizo jana kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Dumila wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Jana, Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo hilo, Asajile Mwambambale, alitangaza kuwa Profesa Kabudi amepita bila kupingwa na kumkabidhi barua ya kuwa mbunge mteule wa Kilosa.

Mwambambale ambaye pia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, alisema hati kamili ya ubunge itatolewa baada ya uchaguzi mkuu kufanyika.

Baada ya kutangazwa kupita bila kupingwa, Profesa Kabudi alisema uamuzi huo unaifanya CCM Wilaya ya Kilosa kuwa na kazi ya kutafuta kura za mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli.

"Leo sijaja kwa ajili ya kampeni, nimekuja tu kuwashukuru kwa kunidhamini," alisema Profesa Kabudi na kuahidi kuwa mtumishi wa wakazi wote wa wilaya hiyo na hatawabagua kwa misingi ya chama, itikadi wala kabila.

## Ulinzi waimarishwa uzinduzi kampeni za CCM Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAANDALIZI ya uzinduzi wa kampeni za urais kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), yamepamba moto huku Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma likiimarisha ulinzi.

Chama hicho kinatarajia kuzindua kampeni zake kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Nipashe ilipita katika mitaa mbalimbali ya jiji hilo jana na kushuhudia kubandikwa kwa mabango ya mgombea urais kupitia CCM, Dk. John Magufuli.

Pia, Mji wa Dodoma umepambwa kwa bendera za chama hicho kwenye mitaa na zingine zikifungwa kwa kamba kutoka upande mmoja wa barabara kwenda mwingine.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Gilles Muroto, alisema jana kuwa wamejipanga kuhakikisha amani na usalama unakuwapo kwenye kampeni hizo.

"Sisi kazi yetu ni usalama wa raia na mali zao, wale ambao wamejifunza hesabu, namba yoyote kipeuo cha sifuri ni moja, umoja wa Watanzania ni amani, utulivu, mshikamano na ni umoja wa kulinda uhuru wa Watanzania," alisema.

Alisema matarajio yao ni kuona vyama vyote vinafanya kampeni kistaarabu kwa kufuata na sheria na kanuni.

"Jeshi limeimarisha ulinzi kuanzia kwenye kampeni mpaka siku ya uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 28, tunaomba watu wajitokeze kupiga kura tarehe ikifika na kurejea majumbani kwao," alisema.

# Madereva bajaji, bodaboda waonywa kushiriki maandamano yasiyo na vibali

**Na Mwandishi Wetu**

MADEREVA wa pikipiki, maarufu kama bodaboda na wale wa bajaji, wameonywa kujiingiza katika maandamano yasiyo na vibali kutoka polisi katika kipindi cha kampeni za uchaguzi.

Onyo hilo lilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, wakati wa kikao cha pamoja na madereva hao kwa lengo la kuwatahadharisha juu ya wanasiasa ambao wanalenga kuwatumia vijana vibaya katika kufanya siasa zao.

Alisema katika kipindi cha hivi karibuni, kumezuka tabia ya baadhi ya wanasiasa kuwarubuni madereva wa vyombo hivyo kwa kuwanunulia mafuta kisha kuwaingiza katika maandamano yasiyo na vibali.

"Hakikisheni hamshiriki katika maandamano ya kisiasa ambayo hayana kibali maalumu kutoka polisi kwani kufanya hivyo ni kinyume cha sheria kwa sababu watawanunulia mafuta lita moja kisha mkajiingiza katika vitendo vya uvunjifu wa sheria," alisema Mutafungwa.

Aliwataka madereva hao kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria na endapo watatakiwa kusafirisha makada wa vyama kwenda katika mikutano ya siasa, wahakikishe hawajiingizi katika vitendo vya uvunjifu wa amani.

Kwa upande wao, madereva hao waliliomba jeshi hilo kusimamia sheria bila upendeleo hasa wakati huu ambao nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu na kubaini wahalifu ambao wanalenga kuichafua kazi yao.

Walisema katika kipindi hiki cha kampeni, baadhi ya watu ambao si waaminifu hujitokeza na kufanya vurugu kwa kutumia pikipiki au bajaji, kitendo ambacho walisema kinachafua taswira ya kazi wanayoifanya.

# Adaiwa kumuua hawara na mtoto kisa mapenzi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Derick Dambuve (26), mkazi wa kijiji cha Mgoma wilayani Ngara kwa tuhuma za kuwaua mama na mtoto wake (2), baada ya mtuhumiwa kukataliwa kimapenzi na mama huyo.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kuwa alifanya unyama huo baada ya kukubaliwa na mama huyo kufanya mapenzi lakini muda mfupi alimkuta akifanya tendo hilo na rafiki yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema jana kuwa wakiwa baa, mtuhumiwa aliwanunulia pombe na baadaye kumuomba rafiki yake aitwaye Alex Kirai ampeleke mama huyo, Helda Amon (28), nyumbani kwake na alimpeleka na kumfikisha salama.

Alisema muda mfupi baada ya kumfikisha na kuondoka alifika rafiki mwingine wa mtuhumiwa aitwaye Kajele Ibrahimu akamtaka kimapenzi akakubali, na wakati wakiendelea kufanya tendo hilo, mtuhumiwa alifika nyumbani kwake juzi saa mbili usiku na kuwafumania.

"Huyu mama alitoroka nyumbani kwa mume wake kijiji cha Muruvangira na kwenda kijiji cha Mgoma anakoishi mtuhumiwa, kulikuwa na gulio akaamua kwenda baa na ndipo akakutana na mtuhumiwa akamtongoza wakakubaliana wakaanza kunywa pombe.

"Mtuhumiwa ni fundi ujenzi na alikuwa na kazi hajamalizia, akamuomba rafiki yake amsaidie kumpeleka huyo hawara yake nyumbani," alisema.

Kamanda Malimi alisema baada ya kufumaniwa rafiki wa mtuhumiwa alikimbia na ndipo mama huyo alianza kushambuliwa hadi kupoteza maisha na kuwa baada ya mtuhumiwa kumuua mama huyo alimuua pia mtoto wake aitwaye Gladness Amon (2) kwa kumpiga na kifaa cha kufanyia mazoezi.

"Mtuhumiwa kutokana na hasira alizokuwa nazo wakati huo, alipomuua mama (hawara yake waliyekutana baa) mtoto alikuwa akilia kwa sauti, akamfuata pia mtoto naye akamuua, inawezekana alitaka kuondoa ushahidi," alisema Malimi.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani wakati wowote baada ya upelelezi kukamilika.



Ofisa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Hussein Omary (kulia), akizungumza kwenye kongamano la taka ni ajira, lililoandaliwa na Jukwaa la Vijana Ubungo, kwa lengo la kuhamasisha vijana wa Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam juzi, kujiajiri kupitia ukusanyaji taka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kukosekana mpango wa ardhi kwaathiri uhifadhi

**Na Salome Kitomari**

KUKOSEKANA kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi kumechangia kwa kiasi kikubwa migogoro baina ya watumiaji wake. Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, Dk. Stephen Nindi, aliyasema hayo hivi karibuni wakati akiwasilisha mada kwa waandishi wa habari kuhusu kulinda uhifadhi kwa kuhakikisha matumizi bora ya ardhi.

Kikao hicho cha mtandaoni kiliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari wa Mazingira Tanzania (JET) kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Alisema uwapo wa mpango wa matumizi bora ya ardhi utasaidia wadau kujipima na kukubaliana kutumia ardhi iliyopo kwa makubaliano pasipo kusababisha migogoro na kulinda uoto wa asili.

"Katika mpango huo ndani ya vijiji utawaleta pamoja watumiaji ambao ni wanakijiji, miji, maeneo yaliyohifadhiwa, hifadhi za Taifa, maeneo ya hifadhi za jamii, ardhi oevu, misitu, maeneo makubwa ya kilimo ya wawekezaji wakubwa na wadogo," alisema.

Aidha, alisema mafanikio yameonekana kwenye vijiji vilivyotekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuhakikisha ulinzi kwa watumiaji wengine kama maeneo ya misitu ya vijijiji, maeneo ya hifadhi ya jamii, vyanzo vya maji na ardhi oevu

Kwa mujibu wa Dk. Nindi, changamoto kubwa kwenye uhifadhi ni kuongezeka kwa shughuli za kilimo, idadi kubwa ya mifugo, ukataji miti, matumizi ya dawa za kilimo na ongezeko la watu.

"Shughuli za kilimo zinaongoza katika kuharibu maeneo yaliyohifadhiwa kwa kuongezeka maeneo ya kilimo, huku maeneo yaliyohifadhiwa yakiendelea kupungua," alisema.

Dk. Nindi alisema jingine ni kukosekana kwa mpango shirikishi wa matumzii ya ardhi katika ngazi ya taifa, mkoa, wilaya na vijiji, umesababisha athari kubwa katika uhifadhi wa viumbe hai. Kwa mujibu wa taarifa iliyopo kwenye tovuti ya tume hiyo, hadi Novemba mwaka jana jumla ya vijiji 23 vya wilaya tiza za mikoa ya Tanga, Ruvuma na Lindi vilikamilisha kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Aidha, kwa ufadhili wa serikali ya Finland kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Divisheni ya Misitu na Nyuki, wanatekeleza mradi wa miaka minne wa kuongoza thamani kupitia mazoa ya misitu na ndani yake miaka miwili ya kwanza ni kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji 57.

Kwa mujibu wa sheria ya upangaji wa matumizi ya ardhi, kila mamlaka itakuwa na haki ya kudhibiti au kuweka mipaka maalum ya ardhi, ugawanyaji wa ardhi, utekelezaji wa mpango wa ardhi, kutunga sheria ndogo za kudhibiti maendeleo na msongamano.

Mengine ni kuhifadhi ardhi yote iliyopangwa kwa ajili ya maeneo ya wazi, yaliyotengwa, ardhi oevu, misitu ya mjini na kanda za uoto, kuasilisha taarifa za athari ya mazingira iliyopitishwa na mamlaka.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tutimize wajibu wetu uchaguzi mkuu

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepuliza kipenga kampeni kwa vyama vyote vilivyosimamisha wagombea udiwani, ubunge na urais kunadi sera zao kwa wananchi kuelekea siku ya kufanya maamuzi Oktoba 28, mwaka huu, ili kuwashawishi kuwachagua kuwaongoza kwa miaka mitano ijayo.

Katika uchaguzi wowote wadau wake ni wananchi, NEC, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Vyama vya siasa, vyombo vya dola, waandishi wa habari na waangalizi wa uchaguzi kutoka ndani na nje ya nchi.

Kipindi hiki ni muhimu sana kwa kuwa ndicho kinaweza kutugawa au kuzidi kutuimarisha kama taifa, na historia inaonyesha nchi nyingi ziliingia katika machafuko nyakati za uchaguzi wa kupata viongozi wa kuongoza kwa kipindi kingine.

Kwa sasa tunachotarajia kutoka kwa wadau wote ni kila mmoja kutimiza wajibu wake katika nafasi yake, akijua dhamana kubwa aliyopewa na nchi kuhakikisha sote tunaendelea kuishi tukiwa nchi moja. Vyama vya siasa vinapaswa kutambua wajibu wa msingi wa kunadi sera zao, kuacha kuzungumzia washindani wao katika kinyang'anyiro, kufanya figisu figisu za kuharibu amani, badala yake kuhakikisha wanaeleweka kwa wananchi ili kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi ndani ya sanduku la kura siku ya uchaguzi.

Lugha za kuudhi, kudhalilisha wengine hazitarajiwi bali wananchi wanataka kusikia ni mgombea akipewa nafasi aliyoomba atawafanyia nini hasa katika kutetea maslahi yao katika Halmashauri, Bunge na nchi. Kwa NEC na ZEC zinapaswa kutoa haki kwa mamlaka zote kwa kusimamia kikamilifu sheria na kanuni za uchaguzi, ikiwamo kutoa taarifa husika kwa umma na kwa wakati ili kuondoa kusambaa kwa taarifa potofu. Haitarajiwi wasimamizi wa uchaguzi ambao halisi ni Wakurugenzi wa Halmashauri na watendaji wa kata, kufanya jambo lolote la kupendelea ili kutoa ushindi nje ya utaratibu.

Kinachotarajiwa ni ratiba ya mikutano ya wagombea kufahamika kwa pande zote kuhakikisha hakuna mwingiliano au kugombana na kuwezesha kupishana katika mikoa na wilaya kwa wagombea kufanya mikutano. Kwa Jeshi la Polisi wajibu wake mkuu ni kulinda raia na mali zao, na kwa kipindi cha uchaguzi wanawalinda wagombea urais, ikiwamo kusimamia usalama kwenye mikutano yote ya hadhara.

Kinachotarajiwa ni kutokuwa na ubaguzi katika utekelezaji wa majukumu yao hasa kwenye muda wa mikutano, ambao umekuwa ukilalamikiwa kwamba wapo wagombea hata wakizidisha muda wa kampeni huachwa kuendelea, huku wengine wakichukuliwa hatua ikiwamo kushushwa kwenye majukwaa.

Kwa waandishi wa habari, wanapaswa kuhakikisha wanatumia kalamu zao vizuri na kutenda haki kwa pande zote, kwamba lazima kipaumbele na uzito wa habari uwe kwa vyama vyote na si kupendelea upande wowote.

Kusiwe na upendeleo wa kutoa muda wa hewani kwa radio na luninga nafasi na mitandao ya kijamii ambayo imepewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Idara ya Habari Maelezo kwa upande wa magazeti. Kwa waangalizi wa ndani na nje, wanapaswa kuhakikisha jicho lao linamulika taratibu, kanuni na sheria za uchaguzi kama zilifuatwa na yaliyojiri kwa kiasi gani yamesababisha uchaguzi kuwa mzuri au na dosari, kisha kutoa ripoti kwa wadau wote na wananchi.

Kwa wananchi wanapaswa kusikiliza kwa makini na kupima hoja za wagombea kama zinatekelezeka, kusoma ilani za vyama na kuhakikisha wanajiridhisha watakayemchagua ndiye atakayekuwa mtu sahihi kutetea maslahi yao katika ngazi za uamuzi.

Mamlaka nyingine ambayo inapaswa kuwa macho TAKUKURU, kwa kuwa katika kipindi hiki ndicho takrima na rushwa nyingine za fedha na mali kwa ajili ya kuwalaghai wapigakura hutolewa, ili anayegombea aweze kupata kura bila kuhakikisha kuwa ana sifa ya kushika nafasi husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanaofanyabiashara kwa ubia wasijisahau, fuatilieni taratibu

Na Mwandishi Wetu

**IWAPO** unakusudia kufanya biashara au uwekezaji ni vyema kuzifahamu kanuni na taratibu ili usije kukwama au kuwa kwenye ukinzani na mamlaka zinazosimamia shughuli hizo.

Ni vyema kufahamu na kuzingatia taratibu na sheria za kuelekeza namna ya kuanzisha na kufanya biashara kwa misingi inayokubalika, mathalani kuandaa jina la biashara, kuisajili, masuala ya kodi na ushuru pamoja na kueleza kwa ufasaha kile unachokusudia kukifanya.

Unapoamua kuwekeza kwa ushirika huna budi kuchunguza kwa umakini wabia unaotaka kujiunga nao, ili kung'amua kama ni watu makini na waaminifu au wadanganyifu.

Pia kama haitoshi, ni vyema ukafanyika mkataba wa maandishi kabla au mapema sana baada ya wahusika kuanzisha biashara kwa ushirikiano.

Hili limshirikishe mwanasheria na mashahidi wengine kwa ufahamu na uhakika zaidi ili kujiepusha au kujikinga na mianya ya kuzidiana ujanja na kudhulumiana.

Kufariki kwa mbia mmoja kunaweza pia kusababisha kuvunjika kwa ushirikiano, halikadhalika, kutokuelewana kwa wabia kunaweza kusababisha kutengana.

Ukiwa na kampuni unatenganisha majukumu ya wamiliki mali na kampuni yaani kampuni inaposajiliwa inakuwa na hadhi na kutambulika kisheria kama ni mfumo tofauti na wamiliki.

Mfumo huu unatenganisha majukumu kati ya menejimenti na wamiliki wa kampuni, madeni ya kampuni yatalipwa hadi kufikia kikomo cha mtaji uliowekezwa na wamiliki.

Hivyo basi, mali binafsi za wamiliki wa kampuni haziwezi kukamatwa kufidia madeni endapo kampuni itafilisika.

Na tena pia, mfumo huu wa kampuni unatoa fursa ya kupanua mtaji kwa kukusanya mitaji kuongeza wanahisa au kupitia soko la mitaji ya hisa.

Mfumo huu ndiyo unafaa kwa biashara kubwa kwani unatoa nafasi ya kupanuka kwa biashara na kuendelea kuwapo kwa biashara hata kama baadhi ya wamiliki wake wakifa au kujitoa kwenye kampuni.

Kadhalika, kuna mambo na vitu muhimu vya kutekeleza kisheria kabla ya kuanzisha biashara kama hivi vifuatavyo, mfano kuwa na ofisi; leseni, kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA), kama mlipakodi na kupewa namba halali (TIN), kufanyiwa makadirio ya kodi ya mapato ya awali na kutimiza masharti mengine ya kisheria.

Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 4(1)(b) na kuendelea cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka, 2008.

Kwa mfano, kama mhusika anataka kufungua kampuni ya ukandarasi ni lazima asajiliwe kwenye Bodi ya Makandarasi.

Na kama anakusudia kufanya biashara ya wastani wa kati au kubwa, kulingana na nguvu ya mtaji, anapaswa kufuata taratibu zote za sheria. Kwani ni kosa kufanya biashara bila kufuata sheria na dhana hii, inatokana na kifungu cha 104(a) na (b) na kile cha 105(a) na (b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato.

Hata hivyo, kuna biashara nyingine ambazo ni ndogo sana, kulingana na kiasi cha mtaji kinachowekezwa na kwamba uanzishwaji wake haulazimu kufuata sheria na taratibu zote tunazozizungumzia.

Kwa mfano, uuzaji vitafunio mathalani vitumbua, vitu vidogo kama pipi, karanga, kashata na ubuyu.

Biashara hizi siyo rasmi au biashara ndogondogo, hivyo basi ni vyema kwa mwekezaji akachunguza kama biashara anayokusudia kuifanya au anayoifanya, kwa jinsi na namna yake, ni ndogo au kubwa ili basi ajue kama inamlazimu kufuata sheria au vinginevyo, zama hizi kuna vitambulisho vya wamachinga navyo ni vyema kuwa nacho.

Kwa mujibu wa kifungu namba 8 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, kutofahamu au kutokujua sheria siyo kinga ya kumfanya mtu asishtakiwe.

## HABARI KITAIFA

# Viongozi serikali ya wanafunzi wafundwa

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, amewataka viongozi wa serikali ya wanafunzi kuwa mfano wa kuigwa kwa kuonyesha nidhamu na maadili kwa wanafunzi chuoni hapo.

Prof. Mwakalila aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi hao wapya wa mwaka 2020/21 na kuwataka wahakikishe wanakuwa na mshikamano, heshima, kuongoza wengine njia sahihi kwa vitendo.

"Heshima ni kitu cha bure, lazima mheshimiane. Kuna wanafunzi wanakuja hapa chuoni wakiwa na umri mdogo hivyo lazima ninyi viongozi muwe mfano wa kuigwa kwa kuonesha nidhamu na maadili yaliyo mema," alisema. Aliwataka wahakikishe wanafuata sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia maslahi ya chuo kwa kutambua kuwa uongozi ni fursa, hivyo lazima wawe wazalendo, wahakikishe wanafanya kazi kwa bidii na wawe waadilifu.

"Kiongozi ana wajibu kwa wanafunzi wenzake ambao wamemchagua, ana wajibu pia kwa chuo, hivyo hakikisheni taarifa mnazozitoa kwa wanafunzi ziwe za kweli na zenye usahihi ili kuepusha migogoro,"Prof. Mwakalila alisema.

Aliwataka wanafunzi kuheshimu wafanyakazi na wenyewe kwa wenyewe kuheshimiana bila kujali umri.

Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Prof. Richard Kangalawe, aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanapanga muda wao ili wafanye vizuri kwenye eneo la taaluma.

"Kazi yetu hapa chuoni ni kusoma na kuhakikisha mnafanya vizuri kwenye taaluma, hivyo jitahidini kupanga vizuri muda wenu ili mfikie malengo mnayokusudia," Prof. Kangalawe.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Elius Mwakalinga (kulia), akikagua barabara ya Rusumo-Lusahunga yenye urefu wa kilomita 92, mkoani Kagera juzi. **PICHA: WUUM**

# Waliopoteza maisha kwa ajali waongezeka

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali iliyolihusisha basi la Sabuni Express wameongezeka kutoka wanane hadi tisa.

Basi hilo lililopinduka katika kijiji cha Kyamalebe likitokea wilayani Muleba kwenda Mwanza Agosti 21, mwaka huu. Idadi hiyo imeongezeka baada ya majeruhi mwingine kupoteza maisha akiwa katika hospitali ya Kagondo wilayani Muleba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alimtaja aliyepoteza maisha kuwa ni Alexandelina Lushoke (55) mkazi wa kijiji cha Kishanda, ambaye alikuwa miongoni mwa majeruhi wanne waliokuwa na hali mbaya.

Alisema majeruhi mwingine amehamishiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Mwanza kwa matibabu zaidi.

Kutokana na hali hiyo, kamanda malimi alisema majeruhi waliobaki wakiendelea na matibabu katika hospitali ya Kagondo inayomilikiwa na Kanisa Katoliki ni wanne tu wengine wameruhusiwa.

Basi la Sabuni Express lilipinduka katika eneo la Kyamalebe na kusababisha vifo vya watu wanane na majeruhi 27 ambao walilazwa katika hospitali za Rubya na Kagondo zilizoko wilayani Muleba.

# Mahakamani tuhuma kujiunganishia umeme

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA Ahmed Khalifa (40) na Abdulrazak Saidi (49) wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, wakikabiliwa na tuhuma za kuingilia miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kujiunganishia umeme kinyume cha sheria.

Wafanyabiashara hao ambao ni wakazi wa jijini Dar es Salaam, walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele.

Upande wa Jamhuri katika shauri hilo uliongozwa na mawakili wa Serikali Waandamizi, Maternus Marandu, Wankyo Saimon na Wakili wa Serikali Benson Mwaitenda.

Marandu alidai kuwa Julai 29, mwaka huu, washtakiwa wakiwa eneo la Mikocheni barabara ya Ndovu, Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwa makusudi waliingilia miundombinu inayotoa huduma muhimu.

Alidai kuwa washtakiwa kwa makusudi walijiunganishia umeme kutoka katika mfumo wa TANESCO na kupitisha pembeni ya mita namba 43153725676 kinyume cha sheria.

Hakimu Matembele aliwaeleza washtakiwa hao kuwa hawatakiwi kujibu chochote kwa sababu wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi na mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza bila kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Marandu alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, lakini umefikia hatua nzuri, kwa hiyo wanaomba tarehe ya karibu kama wiki mbili, utakuwa umekamilika.

Hata hivyo, Hakimu Matembele alisema ili washtakiwa wawe nje kwa dhamana kila mmoja anatakiwa awe na mdhamini mmoja, ambaye atakuwa na barua ya utambulisho na kitambulisho cha taifa au cha kupigia kura.

"Mahakama hii inawataka washtakiwa pamoja na wadhamini wao kutia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano na pia hamtatakiwa kutoka nje ya Dar es Salaam bila kibali cha mahakama, " alisema Hakimu Matembele.

Kesi imeahirishwa hadi Septemba 10, mwaka huu, kwa kutajwa na kuangalia upelelezi umefikia hatua gani. Washtakiwa wamerudishwa rumande kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.

# Wanufaika na mafunzo ujasiriamali

**Na Welingtone Masele,** IGUNGA

ZAIDI ya vijana 100 waliopata elimu ya ujasiriamali Igunga mkoani Tabora wameanza kubadilika baada ya bidhaa wanazozalisha kuvutia wananchi wengi, hivyo kuanza kuwaingizia kipato.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, baadhi ya vijana hao wamemshukuru mwalimu wa ujasiriamali wilayani hapa, Maria Isdori, kwa kuwa elimu waliyoipata imewapa mwanga bora wa maisha.

Stella Moris (25), mkazi wa kata ya Mwanzugi, alisema elimu aliyopata imemwezesha kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo sabuni za kufulia na kuogea, vikapu, vikoi, mazulia na kofia na kuziuza kwa bei nzuri.

Alibainisha kuwa ujuzi huo umempa ajira ya uhakika kwa kuwa sasa anaendesha maisha yake na ameajiri vijana wanne na kupanua mtaji wake. Pia alisema ameanzisha mradi wa ufugaji samaki ambao unamwingizia kipato pia.

Benedicto Joseph (30) na Esta Amos (27) wakazi wa Kata ya Igunga, walisema bidhaa wanazozalisha zinapendwa sana na wananchi ndiyo maana huwa zinanunuliwa zote na kuwaingizia kipato.

Naye Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Grace Nyamwanji, alisema elimu ya ujasiriamali ambayo imekuwa ikitolewa na mwalimu huyo kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri, imewapa vijana ajira za uhakika.

Alibainisha kuwa hadi sasa zaidi ya vijana 200 wameshapewa elimu hiyo. Vijana hao walijifunza jinsi ya kutengeneza mazulia, vikapu, kofia, sabuni za kufuli na kuogea, mikufu, bangili, miradi ya ufugaji kuku, kilimo na ufugaji samaki kwa kutumia teknolojia rahisi na rafiki wa mazingira.

Nyamwanji alimpongeza Isdori kwa moyo wake wa uzalendo na utayari kujitolea kufundisha vijana wenzake elimu ya ujasiriamali na kuongeza kuwa amekuwa msaada mkubwa katika kubadilisha maisha ya vijana wilayani hapa.

Kwa upande wake, Isdori alisema amekuwa akitoa elimu ya kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa kutumia teknolojia rahisi na isiyo na gharama ambayo humwezesha kijana kujiajiri kwa mtaji kidogo tu.

Alibainisha kuwa hadi sasa zaidi ya vijana 100 aliowafundisha wameshaanzisha miradi yao katika maeneo mbalimbali na wanaendelea kunufaika na elimu hiyo.

Hata hivyo, aliishauri serikali kulipa msukumo mkubwa suala la kufundisha elimu ya ujasiriamali shuleni na vyuoni ili kuwezesha vijana wengi zaidi kujiajiri punde wanapohitimu masomo yao na kupunguza ukubwa wa tatizo la ajira hapa nchini.

# Wahitimu wakumbushwa kutoa taarifa sahihi

**Na Joseph Mwendapole**

VIJANA wanaohitimu elimu ya juu nchini wametakiwa kuweka taarifa sahihi kwenye kanzi data ya serikali na kujiandaa ipasavyo watakapoitwa kwa ajili ya usaili wa kazi.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Sekretarieti ya Ajira, Mtage Ugullum, wakati akizungumza na wahitimu wa elimu ya juu.

Wahitimu hao ni wale waliomaliza vyuo vikuu vya nje ya nchi walioungamishwa na Taasisi ya Global Education Link (GEL) na walikuwa wakipewa mafunzo ya namna ya kutafuta ajira kwa mtandao.

Ugullum alisema inashangaza baadhi ya wahitimu kwa makusudi wanaamua kuweka taarifa zisizo sahihi kwenye kanzi data ya serikali na mwisho wake wanakosa sifa ya kupata kazi zinazotangazwa.

"Wewe umesomea shahada ya uzamili ya biashara sasa mle unaweka vitu vingine. Sijui unakuwa unatarajia nini ndugu kwani ukifanya hivyo unakuwa unamdanganya nani na ili unufaike na nini?" Alihoji.

"Kuna tatizo lingine mtu anaomba kazi akipata haendi anasema amepangiwa mbali. Sasa kama uliona ni mbali kwa nini uliiomba? Hapo umewakosesha kazi wenzako waliomba na wakaikosa. kama unaona kazi fulani haikufai usiombe," alisema.

Aliwashauri pia wanapoomba kazi kwenye mfumo kuzingatia maelekezo vizuri na waende kwenye Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) au kwa wanasheria wanaotambuliwa kwa ajili ya kuthibitisha nakala za vyeti vyao.

Wanafunzi hao wanaotarajiwa kuhudhuria mahafali yao Septemba 19, mwaka huu, walikutanishwa jana kwenye mkutano wa siku moja kwa ajili ya kupewa mafunzo kuhusu ajira, uliofanyika kwenye ofisi za GEL, jijini Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yalitolewa na maofisa wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na wale wa Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) ulioko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana.

Mkuu wa Kanda ya Mashariki na Pwani wa TaESa aliyemwakilisha Mkurugenzi wa Huduma za Ajira, Jane Sorogo, aliwaeleza wanafunzi hao malalamiko ya waajiri kwa waomba kazi na malalamiko yanayotolewa na waomba kazi dhidi ya waajiri.

"Tumewafundisha namna mbalimbali za kutatafuta kazi, ni mtu wa aina gani anaajirika kwasababu unaweza kusoma ukawa na cheti lakini huajiriki na matarajio ya mwajiri baada ya kukuajiri na nini kitatokea usipokidhi matarajio ya mwajiri," alisema

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema wanafunzi wanaosoma nje wamekuwa wakilalamika kuwa hukosa pa kuanzia wanaporudi nchini hivyo kuwakutanisha na waajiri na wawekezaji.



Gari maalum kwa ajili ya shughuli za ujenzi likiwa limetumbukia kwenye mtaro katika ujenzi wa barabara ya Shekilango, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bukoba waomba elimu ya miradi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BAADHI ya wakazi wa Kata ya Katerero Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, wameiomba serikali kuwapatia elimu kuhusu jinsi ya kuendesha miradi ya maendeleo kwa jamii ili kuwa na matokeo chanya.

Wakizungumza katika shughuli ya makabidhiano ya mradi wa jamii kati ya Serikali ya Wilaya Bukoba na Shirika la World Vision Tawi la Katerero uliomaliza muda wake, ulikuwa ukihudumia Kata za Katerero, Bujugo, Kanyangeleko na Kemondo, ulihusisha afya, elimu, maji, kilimo ufugaji na uchumi. Johanes Joel, mkazi wa Kata Katerero, alisema miradi inayoletwa inawalenga wananchi kuwabadilisha kwenye maisha na kupiga hatua ya maendeleo kwa kinachokusudiwa.

"Bila kupewa kwanza ufahamu inakuwa vigumu kuyafanya na kuonyesha mwitikio kwani hatuna mwanga wa kuendesha wenyewe na kupata kitu chanya," alisema Joel.

Jeneroza Hamlungi, mkazi wa Kijiji Mlinda Kata Katerero, alisema kuwa na wingi wa miradi kunategemea wananchi kupewa elimu ya kufahamu jambo na kutoka kwenye utegemezi wa ndugu na Serikali. Mkurugenzi wa miradi wa World Vision Tanzania, John Masenza, alisema, mradi wa Kata Katerero umehudumia vijiji 10 na kata nne ambapo umenufaisha watu 390,090.

Masenza alisema, wanufaika wamejifunza shughuli za kilimo, ufugaji ,ujasiriamali, uboreshaji wa afya maji, elimu na kugarimu Sh. bilioni 12.7 kwa muda wa miaka 17 ya mradi huo. Katibu Tawala wa Wilaya Bukoba, Kadole Kilugala, alisema ujuzi uliojengwa kwa wananchi wa kata nne ndani ya wilaya hiyo, utawafaa kipindi chote ambacho shirika halitakuwapo.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu auawa kikatili na mumewe

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Chalantai Kata ya Chala wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Tabita Mwanyanje (29), anadaiwa kuuawa na mumewe kwa kuchomwa kisu shingoni na maeneo mengine ya mwili na mumewe.

Mtuhumiwa huyo, Frank Galimoshi (30), anadaiwa kufanya mauaji hayo kwa kinachodaiwa kuwa ni wivu wa kimapenzi.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justin Masejo, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 25, mwaka huu majira ya saa 10 usiku ulipozuka mgogoro kati ya wanandoa hao, hali iliyopelekea mwanaume huyo kuchukua uamuzi wa kumuua mkewe.

Alisema kuwa mgogoro ulianza pale mwanamke ilipoingia meseji kwenye simu yake ya muhamala wa mshahara ndipo mumewe alipofikiri kuwa meseji hiyo ni ya M-Pesa aliyotumiwa na mwanaume mwingine.

Alisema baada ya kuingia kwa ujumbe huo mfupi kwenye simu ya mwalimu huyo, ndipo mumewe alipohamaki kisha kuanza kumshushia kipigo kisha kuchukua kisu na kuanza kumchoma sehemu mbalimbali za mwili.

Kamanda Masejo alidai baada ya mtuhumiwa kubaini kuwa ameua, naye alianza kujijeruhi kwa lengo la kujiua, lakini ilishindikana, hivyo kukamatwa na alipelekwa hospitalini kwa matibabu na akipona atafikishwa mahakamani.



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkoa wa Shinyanga, Africanus Sulle, akitoa elimu ya usalama barabarani na umuhimu wa kuwa na leseni kwa madereva wa bajaji, pikipiki na wamiliki wa vyombo hivyo, yaliyofanyika mjini Kahama, mkoani Shinyanga, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mtandao kuwabaini wadanganyifu kaya maskini

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) umejipanga kutumia mfumo wa kielektroniki katika kuhakiki na kuzipata kaya maskini kwenye kipindi cha pili cha mpango wa kunusuru kaya maskini wa TASAF III ili kuondokana na kuingiza wasio maskini katika mpango huo na kuwapata walengwa sahihi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema hayo juzi mjini Morogoro katika kikao kazi baina ya wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini na TASAF. Aidha, alisema mfumo huo utawafanya kubaini watu ambao hawana sifa pamoja na wale ambao wameshafariki dunia na kuwaondoa kwenye kunufaika na mpango huo.

Mwamanga alisema TASAF awamu ya tatu kipindi cha pili itatumia kiasi cha shilingi trilioni 2 kwa kipindi cha miaka mine, ambapo itazifikia halmashauri na wilaya 185 Tanzania Bara na Visiwani.

"Katika awamu ya tatu kipindi cha kwanza utekelezaji wake ulifanikiwa kwa asilimia 70, na zilitumika shilingi trilioni 1.7 kwa miaka saba na sasa tunaendelea kuhawilisha," alisema.

Hata hivyo, alisema zaidi ya kaya 1,320 zilijitoa zenyewe baada ya kuona zinajitosheleza kiuwezo baada ya kupokea fedha za uhawilishaji katika kipindi cha TASAF II na III awamu ya kwanza.

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emannuel Kalobero, aliwahimiza waandishi wa habari, kuelimisha wananchi hususani walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini kutumia vyema fursa hiyo adhimu iliyowekwa na serikali kupitia TASAF ili kasi ya kupambana na umaskini iendelee kuwa na mafanikio.

Alisema kwa kiasi fulani inaweza kusemwa mpango wa TASAF umesaidia kuinua uchumi wa nchi na kufikia uchumi wa kati kufuatia walengwa wengi kufikiwa ambao wamezitumia fedha zao katika kuanzisha miradi mbali na kujitegemea kiuchumi.

Pia alisema elimu hiyo isaidie kutoa nafasi kwa wale waliofanya vizuri kujiondoa kwenye mpango kwani huwa kichocheo kwa wengine kuondoka na kupisha wenzao, na kutambua kuwa sio kwamba wanatakiwa kuwa kwenye mpango kwa miaka yote.

# TADB yakipa kiwanda cha nyama mil. 450/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) kwa kutoa mkopo wa masharti nafuu wa shilingi milioni 450 kwa kiwanda cha Meat King Distributors cha jijini hapa na kuziomba benki nyingine ziwape wakulima, wavuvi na wafugaji mikopo ya masharti nafuu pia.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea kiwanda hicho akiwa ameambatana na Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo wa TADB, Jeremiah Mhada, juzi, Waziri Mpina, alieleza kufurahishwa na mkakati wa TADB wa kuinua sekta muhimu za uchumi na kuziomba benki nyingine kuunga mkono azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuviwezesha viwanda vyenye kufanyakazi kwa ufanisi.

TADB imekipa kiwanda cha Meat King Distributors fedha kuboresha miundombinu ili kuongeza uzalishaji na kwa kununua ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe za wafugaji. Waziri Mpina amesifu juhudi hiyo ya TADB.

"Kuwapo kwa kiwanda cha kusindika nyama kama hiki cha Meat King Distributors ni jambo lenye tija kwa taifa kwa sababu usindikaji unaongeza thamani kwa mazao yanayotokana na mifugo na hivyo kuwanufaisha Watanzania wengi wanaojihusisha na kilimo, ufugaji na uvuvi. Naomba benki zote za biashara nchini kuiga mfano wa TADB katika kuwezesha wakulima na viwanda kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu," alisema Waziri Mpina.

Mpina alisema wizara yake itaendelea kuunga mkono wawekazaji katika viwanda ambavyo malighafi zake zinategemea mifugo na kusema wizara yake itahimiza ufugaji wa kisasa utakaomfanya mfugaji anufaike zaidi na mifugo yake.

"Tumejipanga kuendelea kutumia wataalamu wa wizara pamoja na wadau wa mifugo kuhakikisha tunakuwa na mifugo bora ambayo itazalisha nyama bora na kuleta ushindani katika soko la ndani na nje ya mipaka ya Tanzania," alisema.

Mhada alisema mkopo huo mpaka sasa umewanufaisha wakulima wadogo 854 ambao wameunganishwa na soko la uhakika linalotokana na kuwapo kwa kiwanda hicho.

"TADB tunakusudia kuleta mageuzi makubwa katika sekta za ufugaji, uvuvi na kilimo ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malighafi hasa katika kipindi hiki ambamo serikali inatekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema na kuongeza kwamba wanaunga mkono kiwanda hicho kwa sababu ni taasisi inayowahakikishia wafugaji wa Mkoa Arusha na mikoa ya jirani ajira za moja kwa moja na kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

# Sababu za kinadada kumchukia bosi trafiki

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, Africanus Sulle, amesema anachukiwa na baadhi ya wanawake hasa mabinti wasiovaa kofia ngumu wakiwa katika chombo cha moto (bodaboda) kwa visingizio mbalimbali.

Moja ya visingizio hivyo ni kuwa wamesuka na kuogopa misuko yao kuchafuka au kutoonekana kwa watu.

Sulle alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na kutoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa bajaji, pikipiki (bodaboda), baiskeli na wamiliki wa vyombo hivyo katika mkutano wa hadhara uliojumuisha maofisa mipango miji, biashara, TRA , bima , TEMESA, LATRA na mkufunzi kutoka Chuo cha New Vision Driving School.

Alisema kitendo cha wanawake waliosuka mitindo mbalimbali ya nywele kutovaa kofia ngumu wawapo katika chombo cha moto kwa kutaka mitindo hiyo ionekane ni kuhatarisha usalama wao na wanatakiwa kuchukuliwa hatua za kisheria ili tabia hiyo isiendelee kujitokeza.

"Kama utampatia kofia ngumu mwanamke au binti na akakataa kuivaa, hakikisha anaipakata kofia hiyo kisha mpeleke moja kwa moja sehemu ambayo kutakuwa na ofisa wa usalama barabarani kwa hatua zaidi za kisheria, ili kuepuka adhabu zinazoweza kujitokeza ikibainika abiria wako hajavaa kofia," alisema Sulle.

Aliwaka madereva pikipiki kuacha kubeba abiria wengi katika chombo kimoja hasa wanafunzi ambao mwisho wa siku wanaathirika kifua na kuanza kukohoa kwa sababu ya upepo mkali asubuhi waendapo shuleni.

Naye mkufunzi wa udereva mkoani Shinyanga, Deogratus Ezekiel, alisema asilimia kubwa ya ajali zinazotokea maeneo mbalimbali nchini zinasababishwa na baadhi ya madereva waliopata leseni kiujanja ujanja bila kuzitambua alama na sheria za barabarani.

Ofisa wa bima, Hamisi Idd, alisema kuwa Sheria ya Usalama Barabarani Namba 10 ya mwaka 2009 inamtaka mmiliki wa chombo cha moto kuhakikisha anakata bima ya chombo chake kabla ya kuingia barabarani, lakini wengi vyombo vyao havina bima.

Akizungumza kwa niaba ya madereva bajaji na pikipiki, Allex Charles, alisema wamekuwa wakiwapatia kofia ngumu abiria wao, lakini kinadada wanashindwa kuzivaa na kuzishikilia kwa madai watachafua nywele zao walizosuka kwa gharama.

# Wanaharakati watakiwa kutetea maslahi ya wengi

**Na Yasmine Protace**

WANAHARAKATI wametakiwa kufanya kazi kwa kutetea maslahi ya watu wengi badala ya kufanya harakati kwa ajili ya mtu mmoja pekee.

Hayo yalisemwa na mwanaharakati, Selemani Bishagazi, kutoka kituo cha taarifa na maarifa kilichopo Kipunguni jijini Dar es Salaam katika semina za jinsia na maendeleo ya jamii (GDSS) zinazoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP). Alisema mada ambayo ameitoa kwa washiriki hao ni mbinu ya ujenzi wa nguvu ya pamoja katika ufuatiliaji na changamoto ndani ya jamii.

"Wanaharakati wanatakiwa kufanya kazi, kwa kuzingatia mipaka yao na wasipofanya hivyo wanaweza kujiingiza katika migogoro," alisema.

Aliongeza kuwa wanaharakati wanatambua kujua kazi ambazo wanatakiwa kuzifanya, na sio kufanya kazi ambazo zingefanywa na polisi au watu wa serikali za mitaa. Alisema wanaharakati wanatakiwa kuhakikisha wanapinga maduala ya ukatili wa kijinsia, pia mwanaharakati atakiwi kwenda peke yake kufanya kazi za kiharakati na sio kwenda peke yake anaweza kupata matatizo.

"Unapofuatilia jambo omba msaada uende na watu wengine, unaweza kwenda peke yako katika eneo ukajikuta unapata usumbufu hata kupigwa," alisema.

Mwajuma Ally, mmoja wa washiriki wa semina za GDSS, alisema uharakati unatakiwa kufanywa kwa kikundi badala ya mtu mmoja. Alisema baadhi ya watu wanavuka mipaka wa kufanya uwanaharakati na kujikuta wanaingilia kazi zisizo zao.



Mkuu wa Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro, Mathayo Maselle (watatu kushoto), akikata utepe kuashiria ufunguzi rwa tawi la Benki ya NMB Malinyi, juzi. Wengine kutoka kushoto ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mikopo Benki ya NMB, Demetus Kaguna, Kaimu Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Salie Mlay, Meneja wa Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper na Meneja wa Tawi la Malinyi, Ipyana Mwakatobe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakunwa ujio tawi la benki Malinyi

**Na Mwandishi Wetu,** MALINYI

SERIKALI imesema ujio wa Benki ya NMB katika Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro utasaidia kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo kutokana na kuongezeka kwa kasi ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

Sekta zingine zitakazonufaika ni uchimbaji wa madini ya dhahabu ambayo yamegunduliwa hivi karibuni.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Mathayo Masele, wakati akizindua Tawi jipya la Benki ya NMB lililopo wilayani Malinyi, akieleza kuwa ujio wa benki hiyo ulikuwa ukisubiriwa kwa hamu kutokana na kukosekana kwa taasisi yoyote inayotoa huduma za kibenki na hivyo kulazimika kuzifuata huduma hizo kilomita 160 katika mji wa Ifakara wilayani Kilombero.

Alisema benki hiyo licha ya kukuza uchumi, lakini itawapunguzia gharama wafanyabiashara na taasisi za serikali na binafsi ambazo zilikuwa zikitumia gharama kubwa kwa ajili ya kusafirisha fedha kutokana na kuwapo kwa matukio ya uporaji katika barabara kuu ya Malinyi - Kilombero.

Akizungumzia kuhusu fursa mbalimbali, mkuu huyo wa wilaya alisema kuwapo kwa Benki ya NMB sasa kutatoa mwanya kwa wakulima kuzalisha mazao ya biashara pamoja na fursa mpya iliyojitokeza hivi karibuni ya madini ya dhahabu ambayo itaongeza kasi ya ukuaji wa kiuchumi wa wakazi wa Malinyi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Hawa Mposi, alisema walikuwa wakilazimika kutumia wastani wa shilingi 500,000 kwa ajili ya kwenda Wilaya ya Kilombero kufanya mihamala ya fedha ili kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

"Tunawashukuruni sana Benki ya NMB kwa kutusogezea huduma hapa Malinyi, hii itatusaidia sisi kama halmashauri kupunguza gharama tulizokuwa tukizitumia kwa ajili ya kwenda kufanya miamala ya kifedha katika Wilaya ya Kilombero kwa kuwa kulikuwa hakuna taasisi yoyote ya kifedha," alisema mkurugenzi huyo.

Naye Kilongozi Mohamed ambaye mkazi wa Malinyi, alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuwaletea Benki ya NMB kwa kuwa wamekuwa wakilima mpunga kwa wingi, lakini wanapopata pesa mahali pa kuhifadhia ni kilomita 160 kitu ambacho kilikuwa ni hatari kwao kutokana na kuwapo kwa matukio ya uporaji.

Kaimu Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Salie Mlay, alisema moja ya kichocheo kikubwa cha kufungua tawi hilo katika Wilaya ya Malinyi ni kutaka kuwasaidia wakulima na wafugaji waweze kupata mikopo pamoja na elimu ya ushirika utakawapa tija kwa kutumia mfuko wa NMB Foundation.

"Tunataka wakulima wafanye kilimo chenye tija NMB ipo tayari kutoa mikopo kwa wakulima na wafugaji kwa hiyo tumieni fursa hiyo ili kuweza kubadilisha kilimo chenu kiwe chenye tija," alisema Mlay.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper, alisema katika uzinduzi huo unakwenda sambamba na kusaidia jamii ya wana-Malinyi kwa kutoa mabati 135, kofia 12, misumali 76 na mbao 200 kwa ajili ya kukamilisha Shule ya Msingi Nawigo iliyopo Malinyi.



Ukurasa 12

TPDC yaibukia Singida kuvuna mafuta, gesi



Ukurasa 14

## Dawa kuamsha Watanzania utalii wa ndani yagunduliwa

BUFE

IJUMAA AGOSTI 28, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Plastiki ajira 'bwerere' Dar kazi 50,000 papo kwa papo

Ofisa Mazingira, Dk. Hussein Omary (mwenye kipaza sauti), akizungumza na washiriki wa kongamano. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

NI kawaida katika mitaa mingi iwe mijini au kwenye majiji vijana kukaa vijiweni wakisaga meno kulalamikia ukosefu wa ajira.Ni kilio kuanzia Tanga mpaka Tabora, lakini wataalamu wanawaeleza kuwa uchumi na ajira wamevikalia.

Mathalani, Dar es Salaam pekee kuna tani 508 za taka za plastiki zenye thamani ya mamilioni ambazo hazikusanywi kila siku. Hivi wanaolalama wangechangamkia fursa hiyo wakakusanya na kuuza wangekosa ajira?

Ni swali linaloibuka kwenye jukwaa la vijana na ajira likiulizwa na Ofisa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Omary Hussein.

Akizungumza kwenye kongomano la Taka ni Ajira linaloandaliwa na Jukwaa la Vijana wa Ubungo (Ubungo Development Forum), Dk Hussein anasema: ""Dar es Salaam pekee kuna tani 508 za taka za plastiki ambazo hazikusanywi. Hizi zina thamani ya Sh. milioni 175. Kila siku fedha hizo zinapotea kwa vile hakuna wanaozikusanya ili kuzirejeleza (recycling).

Kongamano hilo lililofanyika wiki hii Dar es Salaam na kushirikisha vijana zaidi 200, kwa lengo la kupewa elimu ya kuwawezesha kutumia fursa za ajira zilizopo kwenye maeneo yao.

Ofisa mazingira huyo ambaye alikuwa miongoni mwa wasemaji wakuu, anawaambia vijana kuna fursa nyingi kwenye taka ambazo wanaweza kujiajiri, lakini bado hawajazichangamkia.

**FURSA ZILIPO**

Dokta Hussein anasema, Tanzania inazalisha taka zaidi ya tani milioni 8.7 za plastiki kwa mwaka, huku Dar es Salaam pekee ikizalisha tani 530 kwa siku, lakini zinazokusanywa ni chini ya asilimia 50.

Anawaeleza vijana kuwa hakuna wanaozikusanya kwa ajili ya kuzirejeleza na kuongeza kuwa utafiti uliofanywa sehemu mbalimbali duniani zinaonyesha kwamba asilimia mbili ya wakazi wa mijini wanaweza kujiajiri kupitia taka, lakini kwa Tanzania wanaojitokeza ni wachache na si wengi wanaochangamkia fursa hiyo.

"Utafiti kwa Dar es Salaam unaonyesha kuwa watu waliojiajiri kupitia taka hawazidi 15,000 lakini kuna fursa za ajira 50,000 hivyo takriban 35,000 bado hazina watu, hivyo ni vyema vijana wakachangamkia eneo hilo," anasema Dk. Hussein.

Anafafanua zaidi kuwa Dar es Salaam ina wakazi zaidi ya milioni tano na kuna fursa za ajira 50,000 kupitia taka, lakini waliopo kwenye ajira hiyo ni 15,000 na nyingine 35,000 ziko wazi.

"Kwa upande wa Manispaa ya Ubungo, kuna fursa 20,000 za ajira kupitia taka, hivyo ni muhimu vijana kuziona na kuzichangamkia, na suala la muhimu ni viongozi wa maeneo kuwawekea mazingira wezeshi na bora ili kufanya kazi," anasema ofisa huyo wa mazingira.

Mwenyekiti wa 'Ubungo Development Forum' Peter Christopher, anasema, kwa muda mrefu amefikiria namna ya kuhamasisha vijana kujitosa kwenye ajira za kuzoa taka kwa ajili ya kujiajiri.

"Nilimshirikisha Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, nikawashirikisha pia wataalam wa mazingira hasa Dk. Omary Hussein ambaye alilipokea vizuri," anasema Christopher.

Anaongeza kuwa baada ya hatua hiyo alianza kwa kuzindua jukwaa hilo na Kongamano la Taka ni Ajira kwa kushirikisha baadhi ya vijana ambao walikuwa ni sehemu ya kamati ya maandalizi.

"Vijana niliowashirikisha wanawake kwa wanaume tulipita kila kata kuhamasisha wengine, ambapo zaidi ya 200 wamehudhuria kongamano hili la Agosti 25, mwaka huu," anasema.

Anaongeza: "Lengo lao ni kuhakikisha vijana wa maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Ubungo, wanapata kazi ya kufanya, kuliko kukaa vijiweni, wakati ajira zipo zikiwamo za uzoaji taka, ambazo zinaweza kuwasaidia kuwa na kipato.

"Tunataka kutambuliwa na manispaa kwa kupewa kibali cha kuzoa taka katika mitaa, kwa makubaliano ya kulipwa pesa na wakazi wa maeneo husika na ikiwezekana kwa kutumia magari ya kukodisha."

Anawapa jukumu la kuhamasisha wenzao kwenye maeneo wanayoishi ili kujiunga katika vikundi na kuchangamkia fursa za ajira kupitia taka.

UCHUMI

# TPDC yaibukia Singida kuvuna mafuta, gesi

## • Yafurahia matokeo ya awali • Tayari visima vya majaribio



Miundombinu ya TPDC kwa ajili ya kuvuna na kusafirisha gesi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na John Mapepele,** SINGIDA

UMUHIMU wa mafuta kwenye maendeleo ya Tanzania unaelezwa kuwa ni mtambuka kwa vile kukua kwa sekta ya mafuta kunakuza na kuimarisha maeneo mengine mengi, kuanzia viwanda, ujenzi, usafirishaji, kilimo, biashara na huduma. Ni kwa sababu zote hizo zinategemea mafuta kama nyenzo muhimu ya kuziendesha na kufikia uzalishaji.

Katika jitihada za kuijenga na kuikuza sekta ya mafuta, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) lina mradi wa Eyasi-Wembere, wa kutafutaji mafuta ulioanza mwaka 2015/2016, ambako TPDC ilianza na kukusanya taarifa za awali za utafutaji za kijiofizia za nguvu za uvutano na usumaku (High Resolution Airborne Gravity Radiometry (AGG) Survey Magnetic) na tathmini ya taarifa hizo kufanikisha kuainisha maeneo yenye kina kirefu cha miamba, tabaka la kutosha kuwezesha uzalishaji wa mafuta na gesi asilia.

Matokeo ya taarifa ya AGG yameisukuma TPDC kuendelea na hatua mbalimbali za utafutaji za kijiolojia katika maeneo yaliyoonyesha uwepo wa miamba tabaka lenye mafuta, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio.

Mataragio anafafanua kuwa utafutaji mafuta na gesi unapitia hatua mbalimbali za kitaalamu na kwamba hadi kufikia uchorongaji wa kisima, mwaka wa fedha wa 2019/2020, TPDC ilipanga kuchoronga visima vifupi vitatu katika Bonde la Eyasi-Wembere ambavyo kitaalamu huitwa 'stratigraphic boreholes'. Visima hivyo vilikadiriwa kuwa na urefu wa mita 300 kila kimoja anasema.

> **Mchango wa gesi asilia kwa uchumi wa taifa ni mkubwa kwani fedha zilizookolewa kutokana na matumizi ya gesi asilia takribani trilioni 33 zimeelekezwa katika matumizi mengine katika kukuza uchumi wa nchi anasema Waziri.**



Waziri wa Nishati Medard Kalemani (wa kwanza kulia), akiangalia kazi ya utafiti wa mafuta unaoendelea katika Bonde la Eyasi Wembere: **PICHA: TPDC**

Anasema lengo la kuchoronga visima hivyo vifupi ni kupata sampuli za miamba tabaka kwa ajili ya kufanyia uchunguzi wa taarifa mbalimbali za kijiolojia ili kufahamu ubora na uwezo wake katika upatikanaji wa mafuta na gesi asilia.

Anaongeza kuwa kazi ya kuchoronga ilianza Septemba, 2019 na visima viwili vilichorongwa katika maeneo ya Kining'inila, Igunga na Nyaranja wilayani Meatu. Hata hivyo, kazi ilisimama kutokana na mvua za masika kuwa kubwa na za muda mrefu.

Mara baada ya kufanya tathimini ya kitaalam kwa sampuli zitakazopatikana, TPDC itaendelea na utafutaji wa kina wa mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere kwa kuchukua taarifa za kijiokemia ili kubainisha maeneo yenye mafuta ama gesi asilia na ubora wake.

"Aidha, TPDC inapanga kukusanya takwimu za mitetemo za mfumo wa 2D na baadaye kuchimba kisima kirefu cha utafutaji exploration well." Anasema Mataragio na kuongeza kuwa TPDC kama shirika la umma limedhamiria kufanya kazi hizi kwa kutumia wataalam wake kwa asilimia 100.

Aidha, anasema Kampuni ya Madini ya Taifa (STAMICO) imetoa mitambo kuchorongea na kuzitolea wito kampuni nyingine zinazotoa huduma katika sekta ya mafuta na gesi kuendelee kujiimarisha ili kuweza kufanya kazi za utoaji huduma kwenye sekta hii kama sheria ya petrol inavyotaka kwamba asilimia 25 ya hisa kwa kampuni yoyote lazima imilikiwe na wazawa.

Anakumbusha kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli lina jukumu la kulinda maslahi ya taifa katika sekta ya uendelezaji na utafutaji wa mafuta na gesi nchini na kwamba linawakilisha na kusimamia maslahi ya kitaifa katika sekta ya petroli pamoja na gesi asilia.

Halikadhalika Dk. Mataragio anasema linafanya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi nchini kwa niaba ya Watanzania wote.

Ripoti mbalimbali zinaonyesha kuwa hadi sasa Tanzania haijagundua mafuta lakini imepata gesi asilia pekee na endapo TPDC itafanikiwa kupata mafuta katika eneo hili la Eyasi Wembere, utakuwa ugunduzi wa kihistoria na wenye manufaa makubwa kiuchumi ikiwamo kufanikisha miradi mikubwa ya kiuchumi, kufungua fursa mbalimbali za ajira na biashara ambapo Tanzania itaweza kufanya biashara ya mafuta kimataifa na kitaifa na kurithisha vizazi vijavyo rasilimali hii adhimu.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Zena Said, anaibainisha kuwa, TPDC kama Shirika la Mafuta la Taifa (NOC) kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya 2015 lina jukumu la kufanya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi hapa nchini na nje ya mipaka ya nchi, ambapo katika kutimiza jukumu hili muhimu, imeainisha miradi minne ya kimkakati kwa ajili ya utafutaji mafuta na gesi.

Anaitaja kuwa ni miradi ya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi-Wembere, Songosongo Magharibi pamoja na Kitalu Namba 4/1B.

Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utafutaji. Kipekee Mradi wa Mnazibay Kaskazini ambao uko baharini kwenye kina cha kati uko kwenye hatua za maandalizi ya uchorongaji kisima cha kwanza cha utafutaji mafuta na gesi.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, anasisitiza kuwa endapo Tanzania itafanikiwa kupata mafuta yataifanya isonge mbele kwa kasi kiuchumi na kukamilisha azma ya serikali ya kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa viwanda tofauti na sasa ambapo inategemea mafuta kutoka nje kwa ajili ya nishati ya kuendeshea viwanda.

Kwa mujibu wa Waziri utafiti wa mafuta na gesi asilia katika eneo hili la Eyasi Wembere Kijiji cha Luono unafanywa na TPDC na kuongeza kuwa, utafiti huo ni ndoto ya Rais John Magufuli ya kuona Tanzania inakuwa miongoni mwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki zilizogundua mafuta kwenye maeneo ya kijiografia yanayofanana na bonde hilo la ufa kama ilivyo kwa Kenya na Uganda.

"Uwepo wa TPDC mahali hapa ni utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa Rais Agosti 2016 wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi Chongoleani mkoani Tanga" anasisitiza Kalemani wakati alipokuwa akikagua uchorongaji wa visima vitatu katika eneo hilo.

Anaongeza kuwa anafurahishwa kuona TPDC inachoronga visima vifupi vya utafutaji na kusema hayo ni mapinduzi na mageuzi makubwa kwenye sekta hiyo nchini.

Anawataka kuendelea kutafuta maeneo zaidi kwa ajili ya utafiti huku akitoa wito wa kushirikisha jamii zilizopo kwenye maeneo hayo ili kulinda maeneo hayo na vifaa mbalimbali vinavyotumika.

Utafutaji mafuta na gesi umegundua gesi asilia kiasi cha futi za ujazo trilioni 57.54 ambazo asilimia 60 inatumika katika kuzalisha umeme na matumizi mengine viwandani, kuendesha mitambo, majumbani pamoja na kuendesha magari.

Mchango wa gesi asilia kwa uchumi wa taifa ni mkubwa kwani fedha zilizookolewa kutokana na matumizi ya gesi asilia takribani trilioni 33 zimeelekezwa katika matumizi mengine katika kukuza uchumi wa nchi anasema Waziri.

### WANANCHI WAGUSWA

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Luono ulipo mradi wa Eyasi Wembere, Emmanuel Gengeka, anampongeza Waziri wa Nishati Medard Kalemani na TPDC kuwashirikisha wananchi wa eneo hilo na kuwapatia ajira za muda mfupi ambazo amesema ni msaada mkubwa kwao.


Anakadiriwa kuwa takribani watu 300 watapata ajira za vibarua ikiwa mradi huo utaanza kufanya kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida Dk. Rehema Nchimbi, anamshukuru Rais John Magufuli kwa kazi kubwa ya kuwaletea maendeleo ya kweli wananchi wa Singida akisema imekuwa ni fursa nyingi za uwekezaji kuanzia kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia, madini, korosho na parachichi na kuwataka wawekezaji kufanikisha lengo la kuwekeza Singida.

Anasema licha ya Singida kuwa na fursa nyingi za uwekezaji lakini pia imesheheni vivutio mbalimbali vya utalii na vya kihistoria ambavyo vinaufanya mkoa huo kuwa mahali pekee Tanzania pa kutembelea ukizingatia kuwa ni katikati ya nchi.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# TAKUKURU ikukurukie rushwa kila mahali






NA JOSEPH KULANGWA

TANGU enzi na enzi, familia mbalimbali duniani zimekuwa zikihimiza nidhamu miongoni mwa watu wao na ndiyo sababu hujiwekea taratibu, kanuni na sheria za kuhakikisha zinaishi vizuri kwa amani na ustawi.

Kama si kwa kuunda taasisi au vikundi vya watu na kuwapa dhamana ya kuhakikisha amani hiyo inadumu na kanuni, sheria na taratibu vinafuatwa, basi ziko mila ambazo huzingatiwa na akosaye huchukuliwa hatua sawia.

Hivyo shuleni, katika majumba ya ibada na katika makundi na mikusanyiko yoyote, hapakosekani taratibu hizo na kila akosaye huwajibishwa kwa kuadabishwa.

Hakuna nchi duniani isiyo na vyombo vya kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri na watu wanaishi kwa amani na utulivu, ili kuruhusu maendeleo kufanyika. Kuna majeshi ambayo yameundwa kuhakikisha hayo yanafanyika.

Zipo sheria ambazo husimamia mambo katika familia na pengine koo au makabila, pia shuleni na kwingineko ambako yakishindikana hapo, ndipo huweza kutolewa nje na kupelekwa kwa makundi yaliyo nje ya maeneo hayo.

Mathalan, makosa makubwa kama ya mauaji yakifanyika hata katika familia, Jeshi la Polisi huachiwa kufanya kazi yake ya kupata wahalifu na hatua kuchukuliwa mahakamani.

Makosa kama haya yakiachwa yamalizwe katika ngazi hizo na kidugu, ama huweza kusababisha yaendelee au uamuzi kuchukuliwa kiuonevu na kuangamiza maisha ya walio wengi kwa kisasi.

Kwa hali hiyo, ndiyo sababu kuna makosa ambayo kwa vyovyote vile, huingizwa katika katiba za nchi na kushughulikiwa na vyombo vilivyohalalishwa ndani ya katiba husika.

Tumeshuhudia wanafunzi wanatolewa shuleni na kupelekwa polisi na mahakamani kwa kuzingatia uzito wa makosa, pia ndugu kuondolewa mikononi mwa familia na kufikishwa ngazi za juu za kinidhamu, kwa kuzingatia uzito.

Ikitokea mwanafunzi kaua, hataachiwa mwalimu amcharaze viboko na yaishie hapo. Ikitokea mjomba kamtia mimba mpwa wake, haachiwi mzazi wa binti amwonye na kumkanya na yaishie hapo, la hasha, vyombo vya kisheria vya utoaji haki vitahusishwa.

Inapotokea mhadhiri wa chuo au mwalimu akaomba rushwa ya ngono au fedha ili afaulishe mwanafunzi wake, mambo hayo hayataishia shuleni au chuoni, bali taasisi husika na rushwa itaubeba mzigo huo na kutenda haki.

Nchi inaunda vyombo vyake mahsusi kukabiliana na makosa mbalimbali ya jinai, kama vile Polisi, Uhamiaji, Takukuru na vinginevyo, ili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri na wananchi wanaishi kwa amani na utulivu na kuendelea kuzalisha mali, kwa faida yao.

Vitendo vya mauaji, wizi, ujambazi, ajali, nk. Hujibainisha haraka sana miongoni mwa jamii kuliko rushwa au hongo au ulungula, ambao hufanyika kwa siri kubwa kati ya mtu na mtu au jamii na jamii.

Lakini, serikali huiwezesha taasisi inayopambana na rushwa, kuhakikisha kwamba inakabiliana nayo katika makundi mbalimbali ya kijamii, vikiwamo vyama vya siasa, kampuni na taasisi zingine.

Nchi inapokaribia uchaguzi, taratibu nyingi hufuatwa hatimaye kuhakikisha kuwa umefanyika na kila mmoja ameridhishwa na matokeo na nchi kuendelea na mambo mengine ya kuwaletea maendeleo watu wake, ambao ndio wapiga kura, wachaguaji na wachaguliwa.

Lakini, bado kuna tunaowaamini kwamba bila rushwa mambo hayaendi, bila rushwa hakuna ushindi, hivyo licha ya makatazo, miito na maonyo mbalimbali, bado watu hufanya kila linalowezekana kutoa rushwa na kufanikisha mambo yao.

Kwa kuwa rushwa ni kosa la jinai linalobainishwa katika sheria za nchi, haliwezi kuwa jambo la kuachwa kwa taasisi, kwa imani kwamba italishughulikia kutokana na mipangilio na utaratibu wake.

Kama kosa hili litaachwa hivyo, je, itakuwaje kama makosa mengine kama ya wizi na mauaji yataachwa yashughulikiwe na familia au taasisi zenyewe kwa kuwa tu zina utaratibu wao?

Inawezekana kweli taratibu zikawapo, lakini inategemea na nguvu za taratibu hizo kisheria. Itakuwaje mwanafunzi akimtia mimba mwanafunzi, basi kwa kuwa kuna utaratibu wa viboko basi yaishie kwenye viboko? Tukianza hivi tutamaliza vibaya. Takukuru ishughulikie rushwa bila kuangalia inafanyikia wapi. Alamsiki.

**Simu: (+255) 0713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

BIASHARA

# Dawa kuamsha Watanzania utalii wa ndani yagunduliwa



Vivutio vya watalii ni pamoja na wanyama pori katika hifadhi mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

**Na Joseph Mwendapole**

KUWAJENGEA Watanzania utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii ni jambo linaloweza kuleta matokeo chanya kwenye uchumi kutokana na ukweli kwamba idadi ya watalii wazalendo itaongezeka kwenye maeneo na mapato nayo kuongezeka .

Ni kawaida kuona mbuga za wanyama na vivutio vingine vya utalii nchini vikiwa vimefurika idadi kubwa ya wageni huku wenyeji wakiona kama hizo ni sehemu zisizowahusu.

Katika jitihada za kuamsha umma kutalii na kujiona kama sehemu ya burudani hiyo, taasisi ya Global Education Link (GEL) ambayo huwaunganisha wanafunzi Watanzania kwenda kusoma vyuo vikuu nje inakusudia kuubadili mtizamo huo ili wazawa wafurike kwenye vivutio vya utalii badala ya kuwaachia wageni pekee wafurahie raha zilizoko nchini kwao.

GEL imekuja na wazo la Education Tourism bidhaa itakayoonyeshwa kwenye maonyesho yajayo ya vyuo vikuu maalum yanayotarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga utamaduni kwa wazawa kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo kwenye mikoa mbalimbali.

> **"Inashangaza kuona kuna Watanzania wamefikia utu uzima lakini hawajawahi kufika kwenye mbuga yoyote ya wanyama.**

Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik Mollel, anaiambia Nipashe kuwa utalii ni muhimu ili Watanzania wajue umuhimu wa kwenda kwenye mbuga za wanyama.

Anaongeza kuwa inashangaza kuona kuna Watanzania wamefikia utu uzima lakini hawajawahi kufika kwenye mbuga yoyote ya wanyama.

Anaona kuwa wengi wanaamini vivutio vya utalii ni jambo linalowahusu zaidi wageni na kwamba ndiyo sababu kuna wazee hawajawahi kutembelea vivutio vya utalii.

"Ndiyo maana unaweza kukuta mtu akisafiri kwenda mikoa ya nyanda za juu kusini anawaambia wenzake tukifika Mikumi mniamshe niangalie wanyama na akishaangalia anaenda kusimulia kuwa aliwahi kutembelea wanyama Mikumi wakati aliowaona pale si kwa utalii kwasababu alipaswa kuwaona vizuri na kuwajua kwa undani sifa na tabia zao," anasema Mollel.

Anaongeza kuwa inafaa watu kwenda kuwasoma wanyama hao na kuwajua kwa undani ndipo watakuwa amefanya utalii halisi na ndiyo sababu wageni kutoka mataifa ya nje wanakuja kuangalia wanyama hao baada ya kuwasoma na kuwaelewa.

Shule zinapaswa kuwa na programu za kuwapeleka wanafunzi kwenye mbuga za wanyama ili kuwajengea utamaduni huo ili mwisho wa siku wawe na kiu ya kutembelea mbuga hizo wakiwa wakubwa, anasema.

"Kama ukiwa kwenye basi unasema umetembelea mbuga ya Mikumi basi kusingekuwa na sababu kwa watalii kutoka kwenye mataifa yao kuja kutembelea mbuga za wanyama, wangekaa kwao wakaangalia kwenye televisheni, sasa lazima tujenge utamaduni wa kuthamini rasilimali zetu.Hizi mbuga zina manufaa gani na zitaingizaje fedha bila sisi kuzitembelea," anahoji.

Mollel anasema baadhi ya mambo ambayo Watanzania wanaweza kujifunza wanapotembelea mbuga za wanyama ni kufahamu tabia kama za simba kwamba wanaishi kwa koo na wana maeneo maalum.

"Unapokwenda unajifunza hata kwa faida ya maisha yako binafsi unajua kumbe simba pamoja na ubabe kuna sehemu akifika anakuwa mpole. Unafahamu kuwa wana mipaka na wakiivuka wanazua mapambano makubwa na wenzao," anasema Mollel.

"Viboko pia wana mipaka hiyo na utaambiwa kwanini wanapenda kutembea usiku. Ni sababu zipi zinasababisha wasitoke mchana kuzunguka kama wanavyopenda usiku. Kwanini ukikutana na nyati au faru akiwa akiwa peke yake inakuwa hatari sana kuliko wakiwa kundi? Kumbe tunaweza kujifunza namna Mungu alivyoumba viumbe ambao hawaongei lakini wana busara," anasema Mollel

Anasema elimu ya utalii siyo tu kwa wanafunzi bali kwa watu wa nyanja mbalimbali sekta binafsi na serikalini kujifunza masuala yanayohusu utalii ili wajenge utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii.

Anaeleza kuwa una hifadhi ya taifa ya Nyerere ambayo iko mbele kidogo ya Kisarawe mkoani Pwani ambayo wakazi wa Dar es Salaam wanaweza kwenda kutembelea na kuona wanyama mbalimbali wakiwa na familia zao.

"Wakazi wa Dar es salaam badala ya kutoka na kukimbilia Ngorongoro ambako tunaona kama mbali tunaweza kwenda Kisarawe saa mbili tu na tukaona wanyama wote tukakaa mwishoni mwa wiki tukarudi kwetu, sasa nani anaelimisha watu kuhusu haya yote ndiyo bado ni tatizo ila GEL itafanya hayo" anasema Mollel

Anaongeza kuwa GEL itakuwa idara mpya itakayojikita moja kwa moja kwenye kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kwenda kwenye vivutio vya utalii kwa kutengeneza utaratibu wa kuwapeleka huko mbugani mara kwa mara.

Mollel anasema elimu ya utalii itawajengea watu utamaduni wa kwenda kutembelea vivutio vya utalii mara kwa mara badala ya kutegemea utaratibu wa shule ambao huenda ukawa unafanyika mara chache sana.

"Mfano ukiwa nchini Malaysia kuna mabasi ya kwenda kutembelea Singapore kuiona na kurudi, yaani kuiona tu na kurudi sasa kule kuna miundombinu mizuri na mabasi ya kisasa yanayowapeleka huko na mnarudi kesho yake. Mnapokelewa mnazungushwa mnaonyeshwa Singapore ilivyojengwa kwa ustadi mkubwa sasa kwa raha hizo mtu akifika Malasyia hawezi kuacha kutembelea Singapore," anasema.

"Sisi kwanza tuanze kujenga kiu kwa Watanzania kutembelea vivutio, tukifanikiwa kwenye hilo mahitaji yatakuwa makubwa na wafanyabiashara hasa wenye mabasi watahusishwa kupeleka watu kwenye vivutio vya utalii kama Mikumi. Kule wakifika kuwe na magari maalum ya kuwatembeza na kuwe na kambi za kuchoma nyama, kucheza ngoma za asili na kusikiliza historia ya wanyama, hiyo itasaidia sana kuwajengea kiu ya kwenda huko mara kwa mara," anasema Mollel.





# Mgombea urais CCK aanika sababu za kuenguliwa NEC

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

ALIYEKUWA mgombea wa urais kupitia Chama Cha Kijamii (CCK), David Mwaijojele, amefunguka sababu za kutoteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kugombea huku akidai anahisi kuna hujuma zimefanyika.

Agosti 25, mwaka huu, NEC iliteua wagombea urais kutoka vyama vya siasa 15 kati ya 17 vilivyochukua fomu na mgombea huyo hakuteuliwa kwa kile kilichoelezwa kutokidhi masharti ya tume.

Akizungumza jana ikiwa ni siku mbili baada ya kuenguliwa kwenye uteuzi, Mwaijolele alisema alikuwa na nia ya dhati ya kugombea licha ya kukwamishwa na mgombea mwenza wake, Ali Saidi Juma, na kwamba kutokana na hatua hiyo, hana haja ya kukata rufani.

Alisema mgombea mwenza huyo anapaswa kuhojiwa na waandishi kwa nini alifanya hivyo.

"Anatakiwa mkamhoji kwa nini ulimwangusha mwenzako? Vigezo vyote nimekidhi Tume kasoro kimoja tu cha kukosa mgombea mwenza," alisema.

Mgombea huyo alisema katika utafutaji wa wadhamini, alishirikiana na viongozi wake ambao waligawanyika maeneo mbalimbali ya nchi na yeye alikwenda mikoa mitano.

"Sikutelekezwa na wenzangu bali majukumu yalikuwa mengi na tulikuwa tunasaidiana Tanzania Bara na Visiwani. Wakati nachukua fomu tulikuwa wawili mimi na kaimu mwenezi, wakati wa kurudisha fomu tulipaswa kuwa watu tusiopungua wanne.

"Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na mwenezi kutoka Wete Pemba tulipaswa kuwa nao. Hawa sijaelezwa sababu zaidi ingawa yeye (mgombea mwenza) alipatikana na dharura ya kuumwa ghafla sikupanga mimi mwenyewe nije, bali tulipanga na kukubaliana kwenye chama tuje kwa ajili ya uteuzi," alisema.

Alibainisha kuwa NEC ilieleza utaratibu wake wa kimsingi huku akishukuru kuwa imetenda haki.

"Maana kuna wengine walikuwa wananipiga simu kuniuliza nitakata rufaa (rufani) niende mahakamani. Siwezi kukata kwa sababu kwa sehemu yao tume wamefanya vizuri si kila jambo hadi ushtaki," alisema.

Kwa upande wa chama, alisema wamefanya vizuri kama kuna udhaifu wowote utarekebishwa na kama kuna hujuma watajua namna ya kukabiliana nazo.

"Nahisi kulikuwa na hujuma kwa sababu kitendo kilichofanyika hakuna sababu. Nilipokuwa kwa Jaji niliambiwa kama ni mgonjwa hata kama yupo hospitali gani nitaweza kumfuata, lakini ikashindikana maana Jaji alijua amevuka yupo huku bara, kumbe alisharudi Wete," alisema.

Mwaijojele aliongeza: "Yeye alisema atatoka Wete atavuka na boti ya kwenda Tanga kule kuna ndugu zake na atapanda gari moja kwa moja tukutane Dodoma. Hayo ndiyo makubaliano yangu na mgombea mwenza."

OOO



Msaidizi wa Kiongozi wa Waislam Shia Ithnasheriya, Sheikh Muhammad Abdi (katikati), akikata utepe kufungua huduma ya ugawaji maji bure ya kisima kilichojengwa na taasisi hiyo, eneo la Kigogo Post, jijini Dar es Salaam jana, kuelekea siku ya Ashura ambayo ni kumbukizi kifo cha Imam Hussein (A.S) Mjukuu wa Mtume Muhammad (S.A.W.W). Kushoto ni Mwalimu wa Chuo cha Imam Swadiq (A.S), Sheikh Muhammad Yusufu na mwanafunzi wa chuo hicho, Hemed Tembo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wataka sera, si vijembe na matusi

**Na Mwandishi Wetu**,
DODOMA

WAKAZI wa Dodoma wamewataka wagombea walioteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), katika nafasi mbalimbali kunadi sera za maendeleo badala ya vijembe na matusi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, wananchi hao walisema wana kiu ya kusikia sera zinazochochea maendeleo ili kuamua nani wampe dhamana ya kuongoza.

Mkazi wa Dodoma, Japhet Makau, alisema Watanzania wanategemea uchaguzi utakuwa huru na haki ili yule ambaye wanataka apate nafasi atapata bila migogoro yoyote.

Aliwasihi wanasiasa kunadi sera zenye mashiko kwa wananchi ili kuwapa fursa ya kuchagua kiongozi bora atakayewaongoza. Naye Theojenes Kashasha alisema baada ya mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama na tume kukamilika, sasa ni wakati wa wananchi kusikia sera za wagombea kwenye majukwaa ya kampeni ili kufanya uamuzi sahihi. Kwa upande wake, Haruna Kifimbo alisema uchaguzi wa mwaka huu una upekee mkubwa kutokana na mwamko wa wananchi.

Mchambuzi wa siasa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Biashara (CBE), Tawi la Dodoma, Dk. Nassib Mramba, alisema vyombo vyote vinavyohusika kusimamia uchaguzi vifanye haki kwa watu wote.

"Wananchi pia wanaopelekewa sera katika vyama mbalimbali waamke. Badala ya kusikiliza ushabiki wa kushabikia huyu na huyu, wasikilize wagombea wana ujumbe gani wa kuwaletea maendeleo," alisema.

# Wabunifu 130 waendelezwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema kati ya mwaka 2019 na 2020, wabunifu 130 wameendelezwa na serikali ili ubunifu wao uingie sokoni.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Maofisa Maendeleo ya Jamii na Wathibiti Ubora wa Shule kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara kuhusu maendeleo ya teknolojia na ubunifu nchini.

Alisema wabunifu hao ni kati ya 1,066 walioibuliwa na kutambuliwa na serikali kutoka ngazi mbalimbali hasa za chini.

Pia alisema hadi sasa teknolojia 231 zinazozalishwa vijana wa kitanzania zimetambuliwa kuingizwa kwenye kanzi data ya Taifa.

"Na ubunifu wao uwe wa fursa za kiuchumi kwao na uwe mchango kwenye uchumi wa nchi yetu, kwa mwaka 2019/20 serikali ilitenga na kutoa Sh. milioni 750 kwa ajili ya kuendeleza wabunifu na Sh. milioni 874 zimetengwa kwa ajili hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21," alisema.

Prof. Mdoe alisema serikali inafanya jitihada za kuwatambua wabunifu kuwa ikiwamo tayari imeandaa mwongozo wa kitaifa wa kutambua na kuendeleza ufumbuzi, ubunifu na maarifa asilia.

Pia alisema serikali imeendelea kuboresha uratibu na utaratibu wa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu katika ngazi mbalimbali ili kuhamasisha matumizi ya sayansi teknolojia, uhandisi na hisabati.

"Tumewaleta tushirikiane pamoja kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Alibainisha kuwa serikali inatambua umuhimu wa mchango wa teknolojia na ubunifu katika kurahisisha maisha na kuokoa muda unaotumika kwenye utendaji kazi.

"Ubunifu ni nyenzo na kichocheo cha haraka katika sekta mbalimbali ili kuzalisha bidhaa kwa wingi na kutoa huduma bora zaidi, kila siku tunatumia mashine na mitambo, kuongeza uzalishaji na kipato," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna tatizo la ukusanyaji hafifu wa taarifa za wabunifu kutoka ngazi za kata, vijiji na mitaa na limechangiwa na uelewa mdogo kuhusu dhana ya teknolojia na ubunifu.

"Kwa kuwa kazi ya kutambua teknolojia na Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ni endelevu, wizara imeandaa mafunzo haya kwenu ili kujenga uelewa wa pamoja na kushiriki kikamilifu kuibua wabunifu hasa waliopo kwenye sekta isiyo rasmi na mpo karibu na wananchi," alisema.





# Uboreshaji barabara wakomboa walima tumbaku Chunya

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

WAKULIMA wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya, wamesema uboreshaji wa miundombinu ya barabara wilayani humo, umeanza kupunguza gharama za uzalishaji wa zao hilo, kwa maelezo kuwa kwa sasa gharama za usafirishaji wa pembejeo zimepungua.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakulima hao wa maeneo ya Mtande na Matwiga, walisema awali wakati barabara hazijaboreshwa walikuwa wanachelewa kupata pembejeo hasa mbolea na kwamba hata wakipata walikuwa wanauziwa kwa gharama kubwa.

Josephat Hamza, mkulima na mwanachama wa Chama cha Wakulima wa Tumbaku cha Mtande, alisema barabara ya kutoka Mbeya kwenda mpaka Makongorosi imeboreshwa.

Alisema zamani walikuwa wanachukulia mbolea Mbeya mjini, lakini kwa sasa wanapelekewa mpaka katika maeneo ya vijiji vyao kupitia vyama vya ushirika na kwamba hata gharama sio kubwa kama ilivyokuwa mwanzo.

"Tulikuwa tunanunua mfuko mmoja kwa zaidi ya Sh. 80,000 lakini kwa sasa tunanua mpaka Sh. 48,000 na kwa sasa ni rahisi kwa sababu tunanunua kwa jumla," alisema Hamza.

Alikishukuru Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa zao hilo (CHUTCU) kwa kuwadhamini wakulima hao mikopo ya mbolea na pembejeo zingine za zao hilo.

Naye Hamis Juma, mkulima na mkazi wa Kata ya Lualaje, alisema mwaka huu zao hilo halijawafaidisha kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya hasa mvua kunyesha zaidi ya kiwango kinachostahili.

Alisema mvua hiyo ilikuwa inasababisha mbolea kutofanya kazi na hata wakati wa kuanika jua lilikuwa halitoshi na hivyo baadhi ya mazao yao kuharibika kwa kuwa na rangi ambazo hazitakiwi.

"Tunashukuru sasa hivi tunapata mbolea kwa bei ndogo, lakini naamini tutanufaika zaidi mwakani, mwaka huu tulipata fedha ambazo zilitusaidia tu kulipa madeni," alisema Juma.

Aliiomba serikali kuwasaidia kupata wanunuzi wapya wa zao hilo, ili kuongeza ushindani wa zao hilo na kuongeza bei kwa maelezo kuwa kwa sasa mnunuzi yuko mmoja pekee.

# Makete yaomba hospitali ya wilaya

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

UONGOZI wa Wilaya ya Makete mkoani Njombe, umeiomba Serikali Kuu isaidie ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo kwa maelezo kuwa hospitali iliyopo haina hadhi ya kuwa ya wilaya kutokana na ukongwe wake.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Veronica Kessy, aliyasema hayo juzi alipokuwa anapokea msaada wa lita 200 za rangi zilizotolewa na umoja wa wazaliwa wa wilaya hiyo wanaoishi ndani na nje ya wilaya hiyo ujulikanao kwa jina la Umoja wa Maendeleo Makete (MDA) kwa ajili ya ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje wa hospitali hiyo (OPD).

Alisema hospitali hiyo ilijengwa mwaka 1981 ikiwa kama kituo cha afya, lakini mpaka sasa majengo hayo ndiyo yanayotumika kama hospitali ya wilaya licha ya kuwa baadhi ya majengo yameongezwa na serikali.

Alisema ili kuhakikisha wilaya hiyo inakuwa na hospitali ya wilaya, wameiomba serikali iwasaidie kujenga, na kwamba mchakato umefikia hatua nzuri.

"Tumeshatuma barua ya kuomba Hospitali ya Wilaya katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na tayari ombi hili lilishafika, sasa hivi tunasubiri tupate majibu," alisema Kessy.

Alisema katika wilaya hiyo kuna baadhi ya vituo vya afya ambavyo vina ubora kuliko hata hospitali ya wilaya kwa maelezo kuwa baadhi vinatoa huduma sawa na hospitali hiyo.

Aliwapongeza wanachama wa MDA kwa mchango wao wa rangi kwa maelezo kuwa utasaidia kuboresha jengo hilo la wodi ya wagonjwa wa nje pamoja na maeneo mengine ambayo rangi hiyo itatumika.

Akitoa taarifa ya umoja huo, Katibu wa MDA, Award Mapandilah, alisema lengo la chama hicho ni kuhamasishana kurudi nyumbani kwenda kusaidia shughuli za maendeleo ili kuiendeleza wilaya hiyo.

Alisema awali walikusudia kuisaidia hospitali hiyo vifaa kwa ajili ya kupambana na virusi vya corona, lakini baada ya ugonjwa huo kuonekana umepungua, walijadiliana na uongozi wa wilaya hiyo ili kubadili matumizi.

Alisema baada ya kujadiliana na Mkuu wa Wilaya hiyo walikubaliana fedha hizo zitumike kwa ajili ya kukarabati majengo ya hospitali hiyo ambayo ni kongwe, lakini baadhi ya majengo yamechakaa kutokana na kuwa ya muda mrefu.

"Tunamshukuru sana Mkuu wa Wilaya ambaye tulikubaliana naye kukarabati jengo hili, alituletea mchanganuo wa mahitaji na hivyo tumeleta hivi vitu, tunaomba mkuu uendelee kutuhamasisha ili kila aliyepo mbali akumbuke mjini," alisema Mpandilah.

Alisema wilaya hiyo ina watu wengi ambao ni wasomi na wanakaa maeneo ya mijini ambako wanaishia kuchangia michango isiyokuwa na umuhimu ikiwamo ya harusi na kusahau maeneo waliyotoka ikiwamo hospitali, zahanati na vituo vya afya ambavyo walikuwa wanatibiwa wakiwa wadogo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Makete, Dk. Zakayo Ilomo, aliwashukuru wana Makete hao kwa mchango walioutoa kwa maelezo kuwa utasaidia kuboresha mazingira ya hospitali hiyo.

Aliipongeza serikali pia kwa kuwasaidia kuongeza baadhi ya majengo ya hospitali hiyo na kuifanya iwe angalau na majengo ya kutosha japo hayatoshi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akiendesha moja ya pikipiki zilizonunuliwa na serikali kwa ajili ya maofisa tarafa wa mkoa huo, kutokana na agizo la Rais John Magufuli la kuhakikisha maofisa hao wanapatiwa ili wawafikie wananchi kirahisi, kabla ya kuwakabidhi jijini humo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Pikipiki 17 zamwagwa kwa makatibu tarafa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imekabidhi pikipiki 17 kwa maofisa tarafa wa tarafa zote za mkoa huo, ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kuhakikisha maofisa hao wanapatiwa vyombo hivyo ili kuwarahisishia kuwafikia wananchi.

Akikabidhi pikipiki hizo juzi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mkoa huo una tarafa 15, lakini walinunua pikipiki 17 kwa ajili ya kuiongezea Halmashauri ya Busokelo ambayo ina mazingira magumu na ina uhaba wa magari.

Alisema awali walikabidhi pikipiki saba, na juzi walikabidhi pikipiki 10 na akawataka maofisa hao kwenda kuzitumia kwa ufanisi ili kuwasaidia wananchi na kupunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa na wananchi.

Alisema mara nyingi amekuwa akipokea malalamiko ya wananchi wakimtaka awasaidie kutatua matatizo yanayowakabili hali ambayo inamfanya awe na wasiwasi kuwa wananchi hawana imani na viongozi wa chini.

"Ninyi ni viongozi muhimu sana, mkitekeleza vizuri majukumu yenu mtatusaidia kuunganisha wananchi na Serikali Kuu, pikipiki hizi sio za kutembelea bali ni kuhakikisha mnaweza kufika maeneo ya mbali ambayo hamuwezi kufika kwa miguu," alisema Chalamila.

Alisisitiza viongozi hao kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za nchi ili kuwasaidia wananchi na kupunguza kero ambazo zinawakabili na kuepuka kuzalisha migogoro mipya.


Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema pikipiki zilizonunuliwa zimegharimu Sh. milioni 26, na kwamba awali walikusudia kununua pikipiki 15, lakini wakaamua kuongeza mbili kwa ajili ya Halmashauri ya Busokelo.

Vilevile, alisema wanafanya utaratibu wa kuhakikisha Halmashauri ya Busokelo inapatiwa magari ili kupunguza tatizo la usafiri na utendaji kazi wa viongozi hao badala ya kusubiri bajeti ya Serikali Kuu ya kuipatia magari hayo.

Aliwataka maofisa hao kuhakikisha wanazifanyia matengenezo ya mara kwa mara pikipiki hizo ili kuhakikisha zinadumu kwa muda mrefu na kusaidia kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

"Msije mkawa mnafurahia tu kuendesha bila kuzifanyia matengenezo zinapoharibika, Makatibu Tawala wa Halmashauri muwasaidie kufanyia matengenezo ili kuepuka gharama kubwa," alisema Mtunguja.

Baadhi ya maofisa hao waliishukuru serikali kwa kuwakabidhi pikipiki hizo, huku wakiahidi kuwa watazitumia kwa mujibu wa maelekezo ya serikali hasa katika kuhakikisha wanawafikia wananchi mara kwa mara na kwa wakati.



# Balozi Iddi ahamasisha utalii wa ndani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameitaka Jumuiya ya Waratibu wa Misafara ya Utalii Zanzibar (ZATO), kuendelea kuchukua jitihada kuhamasisha utalii wa ndani na kuacha kutegemea wa nje pekee.

Akifungua mkutano wa pili wa jukwaa la utalii lililofanyika mjini Zanzibar, kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema ni vyema kuhamasisha vijana wa kizanzibari kutembelea vivutio vya ndani.

Balozi Iddi alisema ni jukumu kutangaza haiba na upekee wa vivutio vya utalii vilivyopo na kuacha kuwategemea watu kutoka mataifa mengine kutangaza vivutio hivyo ndani ya nchi.

Alisema Zanzibar inategemea sekta ya utalii kama njia kubwa ya kukuza pato la taifa, huku ikifuatiwa na biashara na za kilimo.

"Mmeweza kutoa uwakilishi kwenye bodi mbalimbali za idara za serikali namna ushirikiano mzuri na Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa pamoja mnaweza kuvitangaza vivutio vya kitalii vilivyopo Zanzibar sehemu mbalimbali duniani," alisema.

Balozi Iddi alisema mwaka 2019, utalii ulichangia Sh. bilioni 833.4 za pato la taifa kulinganisha na Sh. bilioni 712.7 kwa mwaka 2018. Alisema kutokana na takwimu hizo, ni dhahiri kuwa Zanzibar imekosa mapato kwa takriban miezi sita, jambo ambalo litasababisha kushuka kwa pato la taifa na hatimaye maendeleo kuzorota.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kutoa mchango kwa lengo la kufanikisha shughuli mbalimbali za utalii, sambamba na kuwasisitiza kuangalia uwezekano wa kutangaza vivutio hivyo kwenye nchi zingine za Ulaya Mashariki, Asia na Mashariki ya Mbali.

Naye Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mohmoud Thabit Kombo, aliishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mipango kwa kuwahamasisha wafanyabiashara ili kutangaza vivutio vya utalii.

Mwenyekiti wa ZATO, Hassan Ali Mzee, alisema kongamano hilo litatoa nafasi kubwa kwa wadau mbalimbali na kujipanga upya kuboresha utalii kwa kupiga hatua za maendeleo katika nchi.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdalla Mohamed Juma, alisema mikakati ya serikali ni kuendeleza utalii wa ndani na nje kwa kushirikiana na ZATO ili kupata maoni ya wadau na kukutana kwa kutatua changamoto zinazojitokeza katika sekta hiyo.



Baadhi ya viongozi mbalimbali wa dini na serikali wakiwa katika kongamano na mahubiri ya kuombea amani uchaguzi mkuu, lililofanyika viwanja vya Maisara, mjini Zanzibar jana. Kutoka (kushoto) ni Askofu wa Kanisa la Anglikana, Michael Hafidh, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo na Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Marina Thomas. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Matukio ukatili kijinsia yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MATUKIO 114 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa Julai, mwaka huu, huku Wilaya ya Magharibi B ikiongoza ikilinganishwa na wilaya zingine.

Hayo yalibainishwa jana wakati wa uwasilishaji wa ripoti za takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto, katika hafla iliyofanyika Mazizini mjini Unguja.

Akiwasilisha ripoti hiyo, Mtakwimu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ramla Hassan Pandu, alisema miongoni mwa waathirika hao, wanawake walikuwa 29 (asilimia 16.7) na watoto 95 (asilimia 83.3).

Alisema Wilaya ya Magharibi B ilikuwa na matukio 24, ikifuatiwa na Magharibi A (20) na Wilaya ya Mjini (19) wakati Wilaya ya Mkoani ina idadi ndogo zaidi ya matukio ambapo ni mawili tu yameripotiwa.

Ramla alisema idadi ya matukio kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 11.8 kutoka matukio 102 kwa mwezi wa Juni, mwaka huu.

Aliwataja miongoni mwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kuwa waliobakwa ni 56, wanawake walikuwa wanane na wasichana 51 na waliolawitiwa ni 14, kuingiliwa kinyume cha maumbile ni wanne ambao wote ni wasichana.

Alisema watoto wenye umri wa miaka 15 hadi 17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio 46 sawa na asilimia 40.4 ya matukio yote ambayo ni zaidi ya robo moja kulinganisha na miaka mengine ya watoto.

Mtakwimu huyo alisema matukio mengi yanaonyesha yametokea kwa kuwa takwimu zinabainisha kuwa matukio 107 sawa na asilimia 93.9 yamefanyika maeneo hayo kulinganisha na mengine.

Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Uhalifu Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, Inspekta Khamis Mwinyi Bakari, alisema jeshi hilo linaendelea kupambana na wahalifu hao kuhakikisha wanayatokomeza matukio hayo.

"Ni vita vyetu sote, lakini Jeshi la Polisi liko mstari wa mbele kwenye vita hivi. Lengo ni kuiweka nchi kwenye hali ya amani na utulivu," alisema.

# Wanafunzi waonywa kwa vitendo vichafu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MANISPAA ya Magharibi A Unguja imesema inafuatilia kwa karibu tabia na mienendo ya wanafunzi wanaosoma katika shule za manispaa hiyo, baada ya kubaini baadhi ya wanafunzi wanajishughulisha na vitendo vichafu.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Amour Ali Mussa, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na kamati ya wazee, walimu na wanafunzi wa Shule ya Kama, huku akiweka wazi uwapo wa wanafunzi wanaofanya mambo kinyume cha maadili.

Kauli ya mkurugenzi huyo imekuja kutokana na kukamatwa kwa wanafunzi na CD zenye video na picha za ngono sambamba na wengine kukamatwa wakiwa na vidonge vya uzazi wa mpango.

Alisema uongozi wa manispaa yake utafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha wanaendeleza mapambano na wanafunzi wawe makini baada ya kukutwa na vitu hivyo vikiwamo mafuta mazuri.

Aidha, alisema juhudi za pamoja kati ya walimu, wazazi na watendaji wa manispaa zinahitajika katika kusimamia vyema vijana na kuwajenga kimaadili ili kupata elimu.

"Wanafunzi hapa mmefuata elimu, mambo yasiyofaa hampaswi kuyafanya wakati wenu bado, tutakayembaini anajihusisha na vitendo visivyofaa, tutamchukulia hatua ikiwamo kumfukuza skuli (shule)," alisema.

Pia alisema kutokana na changamoto zilizobainika, baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo watalazimika kupelekwa kwa wataalamu wa afya ili wakapimwe ujauzito, hususani wanafunzi wa kidato cha tatu.

"Hapa walimu na wazazi kwa tatizo hili lilivyo naomba tuungane pamoja tutumie wataalamu wetu tuwaangalie hali za afya zao vijana wetu kama wapo salama na tuhakikishe tunashirikiana zaidi na kuwa karibu nao muda wote," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Wazee wa Shule ya Kama, Khamis Ali Khamis, aliwataka wanafunzi kutojihusisha na vitendo vya anasa badala yake kujishughulisha na masomo ili kujijengea mazingira bora ya maisha yao ya baadaye.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi kwa na biashara. **Mawasiliano: 0757 079057.**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**Leticia Benard** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **S.0380-0012** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 katika shule ya Sekondari Chama na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0631-0010** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007 katika shule ya Sekondari Umoja. Yeyote atakeiviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DSM/PHQ/RB/618560/2020**

115876402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**KATIKA MAHAKAMA YA CHAMWINO MJINI WILAYA DODOMA MJINI**

**MADAI NAMBARI 375/2019**

**Mdai GEORGE H. URIYO**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa GEORGE KISEGO**

**KWA GEORGE KISEGO – DAR ES SALAAM MWENYEKITI WA MTAA TABATA.**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba Tsh 12,000,000. Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku jumatano tarehe 09/09/2020 saa mbili asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama haukuhudhuria siku tajwa tajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kuwa umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 24/8/2020.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

115876702

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ANNA YOHANA MBELWA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **Suzuki - ESCUDO.** Yenye namba za Usajili **T739 AJZ .** Chassis - **TDO1W206978.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa Polisi :

**DAR/BUG/RB/624191/2020**

115876502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI S.M.M 1984 NYONGEZA KANUNI 2**

**Katika mahakama ya Mwanzo Dodoma Mjini**

**Usimamizi wa Mirathi 1001/2020**

**Ombi la SALOME ELIREHEMA kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu Manyussi William Kyando**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 4.09.2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/08/2020.

Sahihi ya Hakimu

115876602

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BUKOBA, KAGERA**

**RUFAA NA . 41/2020**

**DEOGRASIAS ANATORY.................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**STEPHANO JOSEPH.................................MRUFANIWA**

**KWA: STEPHANO JOSEPH (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na. 41/2020 imepangwa kutajwa tarehe 24.09.2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza ,R.MTEI saa 2:00 asubuhi, mahali-Bukoba Mjini.

Hivyo ,unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 19.08.2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA

115875602

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ASAJILE BROWN KAJUNI** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye chassis namba zifuatazo, **LTB8GBJ2K01524** na **LTBPK8BGOJ2KO8092** na **L7GPCJLY7H1128497.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi

**MBE/MBE/RB/ 618832/2020.**

215874902

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Kundi Kitinga Felix** Wa mjini kati Kahana,anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 475 APH.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake

Taarifa ya Polisi.

**KAH/TR/RB/1289/2020.**

215875002

---

## KUFUNGWA KWA KAMPUNI

**WAMILIKI WA KAMPUNI YA JARMAK COMPANY LIMITED** NAMBA YA USAJILI **132892** YA TAREHE **1 FEBRUARI 2017.** WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA.

215875202

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EMANUEL AIKAEL anatangaza** kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T621 CVR** aina ya **TOYOTA VITZ** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya Polisi:

**DAR/SEL/RB/549884/2020**

215875102

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENEDICT EMMANUEL KYASS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T586 DHX** aina ya **TOYOTA RAV4** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya Polisi:

**DAR/OST/RB/621228/2020**

115876002

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba ya usajili **MC 105 CAG** aina ya **BAJAJ BOXER** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya Polisi:

**DAR/CHA/RB/323849/2020**

115876202


*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mgombea udiwani CCM afariki dunia

**Na Francis Godwin,** IRINGA

ALIYEKUWA Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Iringa, Onesmo Mtatifikilo ambaye alikuwa ni mgombea udiwani wa Kata ya Idodi Jimbo la Isimani kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), amefariki dunia akiwa katika matibabu.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, Katibu wa CCM Wilaya ya Iringa Vijijini, Mobutu Malima, alisema kuwa Mtatifikolo alianza kulalamika kuumwa juzi wakati wa kurejesha fomu ya udiwani na baada ya hapo aliendesha gari lake na kurejea kijijini kwake Idodi.

Alisema kuwa baada ya kufika Idodi inadaiwa hali ilibadilika zaidi na hivyo kulazwa katika Kituo cha Afya Idodi kwa matibabu zaidi kabla ya kumhamishia katika Hospitali ya Ipamba ambayo ni Hospitali Teule ya Wilaya ya Iringa kwa matibabu zaidi.

"Hadi jana jioni (juzi) tulikwenda kumtazama katika Hospitali ya Ipamba tukiwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi, ambaye ni mgombea ubunge wa Jimbo la Isimani... tulifika na kumkuta akiwa katika chumba cha wagonjwa mahututi, japo tuliweza kumwona na kumjulia hali," alisema.

Alisema kuwa taarifa ambazo alizipata usiku majira ya saa 10 ni kuwa mgombea huyo amefariki dunia, jambo ambalo limemsikitisha zaidi na kuwa chama kimekwishaijulisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) juu ya kifo cha mgombea huyo.

Wakimzungumzia mgombea huyo, Stevin Mhapa mgombea udiwani Kata ya Kalenga na Shakra Kiwanga walisema kuwa kifo cha diwani huyo kimeacha pengo kubwa kwa halmashauri hasa ukizingatia enzi za uhai wake marehemu alikuwa ni kiongozi wa maendeleo zaidi.



Mchuuzi akijiandaa kujitwisha beseni lenye maparachichi, tayari kwa kuanza kusaka wateja katika Barabara ya Selander, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Magufuli atekeleza ahadi ya Kilosa

**Na Mary Geofrey,** KILOSA

RAIS John Magufuli ametekeleza ahadi yake ya kupanua eneo la wafanyabiashara ndogo ndogo wa Dumila wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Agosti 5, mwaka huu, Rais Magufuli akiwa njiani kuelekea jijini Dodoma, akitokea Dar es Salaam, alielezwa kilio cha wajasiriamali hao kuomba kuongezewa eneo la kufanyia biashara za matunda na mboga na kuahidi kutoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya ukarabari wa eneo lote.

Nipashe jana lilipitia eneo hilo na kushuhudia shughuli za ujenzi zikiendelea katika sambamba na magari yenye vifaa vya ujenzi yakiwa yamepaki kwa ajili ya kushusha mizigo.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, mgombea ubunge wa jimbo la Kilosa, Profesa Palamagamba Kabudi, alimshukuru Rais Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake na kwamba kazi inaendelea kwa kasi.

Akiwa eneo la kata ya Dumila katika ziara yake ya siku moja ya kuwashukuru wana CCM na wananchi wa jimbo hilo kwa kumdhamini kuwania nafasi hiyo, alisema tayari Serikali imeanza kufanya kazi ya kupanua eneo hilo la biashara.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutawafanya wafanyabiashara wa eneo hilo, kufanya shughuli zao kwa uhuru na kuwa katika miundombinu salama na yenye ubora.

"Wakazi wa Dumila na wilaya ya Kilosa tuna kila sababu ya kumshukuru Rais Magufuli kwa kutoa fedha za kujenga eneo la wafanyabiashara ili kuondokana na changamoto waliyokuwa wakiipata awali," alisema Profesa Kabudi.

Alisema ni matumaini yake mradi huo utakamilika kwa wakati ili uanze kutumiwa na wafanyabiashara hao kwa ajili ya kupendezesha mji wa Dumila na wilaya ya Kilosa.

Awali wafanyabiashara hao, walimuomba Rais Magufuli awaongezee eneo lililopo kando ya barabara ya kuelekea mkoani Dodoma ili walitumie kufanya biashara zao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema wanaomba eneo la shamba lililo karibu na barabara ya kuelekea Dodoma wapewe kwa ajili ya kuongeza sehemu ya kufanyia biashara.

Rais Magufuli amepitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwania tena nafasi ya urais kupitia CCM, huku akishindana na wagombea wengine 14 wa vyama upinzani.

# TPSF yahamasisha vijana kilimo cha matunda, mboga

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), imesema kuwa mboga na matunda vina soko la uhakika ndani na nje ya Tanzania, hivyo vijana wakilima mazao hayo watajiajiri haraka na kuushinda umaskini kwa kiasi kikubwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPSF, Angelina Ngalula, ndiye aliyebainisha fursa hiyo alipokuwa akizungumza na wakulima wadogo baada ya kuvutiwa na mashamba yao ya mboga na matunda katika Kijiji cha Mazombe. Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa na pia kusikiliza changamoto zinazowakabili.

Aliwataka vijana wa Tanzania kulima mboga na matunda na kutokana na adha ya umasikini.

"Mboga na matunda vina soko kubwa sana nje ya nchi hususani nchi za Ulaya. Jukumu letu kuzalisha na kupeleka mzigo mingi nje ya nchi na kuleta fedha ya kigeni nchini," alisema Ngalula na kuwaomba vijana wajiingize katika kilimo hicho.

Alisema moja ya changamoto kubwa nchini ni kilimo cha mazoea ambacho kinatoa mazao yasiyokidhi ubora soko.

Amewapongeza wakulima wa Mazombe na kuahidi kuwapeleka wataalum kutoka Chama cha Wakulima wa Mboga na Matunda Tanzania (TAHA) ili wawape ujuzi unaotakiwa na kuinua kipato chao.

"Niwaomba vijana, hasa wanawake, mjiunge katika vikundi ili muweze kufikiwa kwa urahisi na watoa huduma mbali mbali, ikiwa ni pamoja na taasisi za kifedha zinazoweza kuwapa mikopo," alisema Ngalula.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Hassan Ally Kikoti, aliiomba TPSF iwaunganishe na taasisi za kifedha ili kukopeshwe na kuendelea kilimo chao.

"Changamoto kubwa tuliyonayo ni mitaji ya kuendeleza kilimo cha mboga. Kwa kukosa fedha tunazalisha kidogo kuliko mahitaji ya soko," alisema Bw.Kikoti

Mmoja wa wakulima, Bw Alex Msumile, alisema kilimo kweli kinatoa ajira, lakini akaongeza kwamba wanakabiliwa upatikanaji wa masoko ya uhakika na bei nzuri kwa mazao yao. jambo ambalo limekuwa likiwarudisha nyuma kimaendeleo.

**Changamoto kubwa tuliyonayo ni mitaji ya kuendeleza kilimo cha mboga. Kwa kukosa fedha tunazalisha kidogo kuliko mahitaji ya soko.**

# Lukaku awatuliza mashabiki Inter Milan

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku ameandika waraka kwa mashabiki wa timu yake ya Inter Milan akisisitiza kuwa atarejea kwa kishindo baada ya bao lake la kujifunga kuigharimu timu hiyo kukosa taji la Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester United alifunga bao katika fainali hiyo, lakini zikiwa zimebaki dakika 15 kabla ya mchezo kumalizika na matokeo yakiwa 2-2, Lukaku alijifunga.

Raia huyo wa Ubelgiji alionyesha kujutia kosa hilo kiasi cha kushindwa kwenda kuchukua medali yake ya mshindi wa pili.

Lakini katika posti yake ya kwanza kwenye mitandao ya kijamii tangu fainali hiyo, Lukaku amewaahidi mashabiki wake kuwa atarejea kwa kishindo.

Lukaku aliandika kwenye Instagram: "Kwanza napenda kuwashukuru wote kwa kile mlichokifanya kwa familia yangu na kwangu mwenyewe.

"Mwaka huu kama timu tumekuwa pamoja na ni heshima kuiwakilisha klabu niliyoipenda tangu nilipokuwa mtoto. Ndiyo, kilichotokea kwenye fainali kilinihuzunisha, lakini nitapambana tena.

"Hakuna kitu rahisi katika maisha kama wengi mnavyojua na uzoefu huu utanifanya niwe imara zaidi."







# CHILWELL SASA NI MALI YA CHELSEA

**LONDON,** England

CHELSEA imekamilisha usajili wa mlinzi wa kushoto wa timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell kutoka Leicester City.

Nyota huyo ametua hapo Stamford Bridge kwa mkataba wa miaka mitano huku uhamisho wake ukigharimu kiasi cha pauni milioni 50.

Chilwell anakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na Chelsea baada ya winga wa Algeria, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 27, akitokea Ajax ya Uholanzi na mshambuliaji Timo Werner mwenye miaka 24, kutoka RB Leipzig ya Ujerumani.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 23, ni zao halisi la Leicester City ambapo alipata nafasi ya kwanza kucheza klabuni hapo mwaka 2015, lakini aliingia kwenye mkataba na Mbweha hao mwaka 2014.

Msimu uliopita wa 2019/20, beki huyo alikosa mechi tano za mwisho kutokana na kuwa majeruhi ingawa sasa amepona.

Chelsea walimaliza Ligi Kuu ya England wakiwa nafasi ya nne kwenye msimamo, juu ya Leicester City ambayo imeshika nafasi ya tano.

"Naangalia changamoto mpya, kama kijana nataka changamoto, Naamini hapa nitaipata na nina furaha kubwa kuwa sehemu ya kikosi na chini ya Frank Lampard," alisema Chilwell baada ya kutia saini mkataba na Chelsea.

Chilwell ameichezea Leicester mechi 123 na kufunga mabao manne.

# *Maguire hatarini kuvuliwa unahodha Manchester United*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inafikiria uwezekano wa kumvua unahodha mlinzi wao wa kati, Harry Maguire baada ya kukutwa na hatia katika kesi iliyokuwa inamkabili ya kujaribu kutoa rushwa na lugha ya jeuri kwa polisi wa Ugiriki.


Jumanne Mahakama ya Ugiriki ilisema Maguire ambaye alijiunga na United akitokea Leicester City mwaka 2019, atatakiwa kutumikia kifungo cha nje cha cha miezi 21 na siku 10.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ana uwezekano mdogo sana wa kuendelea kuwa nahodha wa kikosi hicho kwa msimu ujao.

Taarifa ya klabu ilisema: "Haina hofu na kesi ya Maguire kwani rekodi zinaonyesha hana makosa kama hayo ambayo amewahi kuyafanya". Mchezaji huyo raia wa England alitajwa kuwa nahodha wa kudumu ndani ya United Januari akichukua nafasi ya Ashley Young ambaye alijiunga na Inter Milan.

Mwanasheria wa mchezaji huyo amesema licha ya hukumu kutolewa bado Maguire anaweza kuwaomba radhi Ugiriki na polisi.

Mapema Jumanne, Maguire alitajwa kuwa sehemu ya kikosi cha taifa cha kocha Gareth Southgate ambacho kinajiandaa na mchezo dhidi ya Iceland na Denmark, lakini baadaye aliondoshwa kutokana na kesi hiyo.



# VARDY ASAINI MIAKA MITATU LEICESTER CITY




**LONDON,** England

MSHINDI wa Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi Kuu ya England, Jamie Vardy, amesaini mkataba mpya wa miaka mitatu na Leicester City.

Straika huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England amekuwa mchezaji muhimu sana tangu ajiunge na Mbweha hao akitokea Fleetwood Town mwaka 2012, akichangia kwa kiasi kikubwa wakati wakitwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England msimu wa 2015-16.

Vardy alikuwa bado na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, amekubali kuendelea kubaki hapo kwenye Uwanja wa King Power kwa misimu mingine mitatu zaidi.

"Safari niliyoanza nayo na klabu hii ni ngumu kuielezea, na sasa tumekuwa pamoja kwa muda mrefu, ni hisia za aina yake kuingia tena mkataba mpya na Leicester City," alisema Vardy akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Napenda kucheza soka mbele ya mashabiki wa uwanja wa King Power na nina shauku kubwa ya kuendelea na safari hii katika klabu ninayoipenda.

"Tuna timu ya kuvutia na ninaamini tuna uwezo wa kufanya mambo yakawa bora zaidi na nipo tayari kusubiri hilo na kuona kitu gani tutakachokipata kwa miaka michache ijayo."

Vardy msimu uliomalizika alifunga mabao 23 kwenye Ligi Kuu katika mechi 35 alizoichezea timu hiyo inayonolewa na kocha, Brendan Rodgers, ambayo ilimaliza nafasi ya tano kwenye msimamo.

## Ibrahimovic bado ajivutavuta AC Milan

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic bado hajafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na AC Milan, amesisitiza wakala wake, Mino Raiola.

Ibrahimovic alirudi pale San Siro Januari baada ya mkataba wake na Los Angeles Galaxy kumalizika na amefunga mabao 11 katika mechi 20 alizowachezea Rossoneri hao.

Hata hivyo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 38, hayupo kwenye mkataba mpya wa kuitumikia timu hiyo msimu ujao.

Ripoti za nchini Italia za Jumatano zilidai kwamba makubaliano yameshafikiwa, huku Ibrahimovic akijatwa kukubali kusaini mkataba wa mwaka mmoja kwa mshahara wa euro milioni sita.

Lakini Raiola haraka aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter na kukanusha madai hayo.

"Ibrahimovic hajasaini mkataba mpya na AC Milan," aliandika wakala huyo na kuongeza; "taarifa hizo ni za uzushi."





## Southgate awatabiria makubwa Foden, Greenwood England

**LONDON,** England

PHIL Foden na Mason Greenwood wanaweza kuwa nyota wa muda mrefu wa timu ya Taifa ya England, kwa mujibu wa kocha wa kikosi hicho, Gareth Southgate.

Wachezaji hao vijana wa Manchester City na Manchester United waliitwa kwa mara kwanza kwenye timu ya Taifa ya England pamoja na kiungo wa Leeds United, Kalvin Phillips, wakati Southgate alipotaja kikosi cha wachezaji 24 kinachojiandaa na mchezo wa mashindano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Iceland na Denmark.

Mabao matano kati ya sita ya Foden kwenye Ligi Kuu ya England alifunga mara msimu uliporudi baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. Na tangu hapo kocha wake, Pep Guardiola amekuwa akitoa nafasi ya kucheza mara kwa mara kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

Greenwood alijiwekea rekodi yake kwa kufunga mabao 17 kwa msimu mmoja kwenye mechi za mashindano yote alizocheza msimu wa 2019-20 - akifikia rekodi za magwiji George Best, Brian Kidd na Wayne Rooney ambao walifunga idadi hiyo ya mabao kwa msimu mmoja wakati wakiwa na umri mdogo.

"Wote wawili wamekuwa na kiwango cha kuvutia sana kwenye timu zao," alisema Southgate akinukuliwa na waandishi wa habari.

"Wote wamecheza mechi kubwa, mechi muhimu katika klabu kubwa na walikuwa na mchango mkubwa.

"Wana nafasi kubwa ya kuwa nyota wa muda mrefu sana kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAYUPO WA KUMNUNUA MESSI SASA-RAIS MADRID

●●● Ada ni kitu ambacho mnaweza kuafikiana ila hakuna atakayelipa euro milioni 700...

**BARCELONA,** Hispania

RAMON Calderon, Rais wa zamani wa Real Madrid, anatarajia Barcelona itakubali kupunguza ada ya uhamisho "isiyolipika" kwa nahodha wake, Lionel Messi.

**Messi ameomba kuondoka Barca – ikiwa ndio klabu pekee aliyoichezea kwa kipindi kirefu cha maisha yake ya soka baada ya kuwa na msimu mgumu pale Camp Nou ambapo walishindwa kutwaa taji lolote msimu uliomalizika.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, anakipengele kwenye mkataba wake ambacho kinamruhusu kuondoka klabuni hapo akiwa mchezaji huru kila mwishoni mwa msimu.

Imedaiwa kwamba, Messi anataka kutumia kipengele hicho ili kuondoka, lakini Barca imeripotiwa kwamba haiko tayari kwa hilo kwani kipengele hicho kilishamalizika muda wake Mei mwaka huu.

Hivyo, klabu inayotaka kumsajili Messi inatakiwa kulipa kiasi cha euro milioni 700, ada ambayo inaonekana kuwa ni ngumu kwa klabu kuilipa hasa kutokana na uchumi wa soka la dunia kutingishwa na janga la mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini Calderon, anaimani kwamba, Josep Maria Bartomeu atakubali kuipunguza.

"Nina uhakika kabisa watafikia makubaliano ya kirafiki," alisema Calderon akiiambia Stats Perform News. "Wamekuwa pamoja kwa miaka 20.

"Messi amejitoa kwa ubora wake wote Barcelona, na Barcelona wamempa kila kitu Messi. Wameshinda mataji mengi pamoja. Messi ameshinda Ballons d'Or mara sita akiwa pale.

"Nashawishika kwamba watafikia makubaliano ya kiurafiki na kila kitu kitakwenda sawa. Hata ningekuwa mimi ningejaribu kufanya hivyo na nina imani Bartomeu (Rais wa Barcelona) atafanya hivyo hivyo.

"Namjua vizuri. Ni mtu mtulivu, na ataangalia suluhisho bora kwa pande zote mbili. Hakuna haja ya kwenda kwenye mambo ya kisheria."

Mshahara wa Messi pia unaweza kuwa kikwazo kingine kwa klabu itakayomtaka, lakini Calderon anaamini mshambuliaji huyo lazima alipwe kiasi kikubwa kutokana na thamamni yake.

Juventus walilipa euro milioni 100 kwa Madrid kwa mpinzani mkubwa wa Messi, Cristiano Ronaldo miaka miwili iliyopita, ada ambayo Calderon anaiona ilikuwa ya makubaliano.

"Ni kweli kwamba ana umri wa miaka 33, lakini Messi bado ana uwezo wa kutamba kwa miaka mingine mitatu au minne.

"Sijui, lakini ada ni kitu ambacho mnaweza kuafikiana na kuelewana. Nina uhakika hakuna mtu atakayelipa euro milioni 700 kwa wakati huu."

## ZISIKUPITE

### CAVANI AIKATALIA JUVENTUS

EDINSON Cavani, 33, amekataa kujiunga na Juventus kutokana na uaminifu wake kwa klabu yake ya zamani ya Napoli. Nyota huyo wa Uruguay aliondoka Paris St-Germain mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Mail)***

### BABA MESSI ATUA MAN CITY

BABA yake Lionel Messi tayari yupo nchini England kujadiliana dili la miaka miwili na Manchester City baada ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 33, kusema anaondoka Barcelona. ***(Sun)***

### AAMBIWA ATAFUTE TIMU

NYOTA wa Barcelona na Uruguay, Luis Suarez, 33, aliitwa na kocha mpya, Ronald Koeman Jumatatu na kumwambia anatakiwa kutafuta klabu mpya. ***(Mail)***

### THIAGO APIMWA AFYA CHELSEA

MLINZI wa Brazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 35, jana Alhamisi alifanyiwa vipimo vya afya mjini Milan nchini Italia tayari kwenda kujiunga na Chelsea akitokea Paris St-Germain. ***(Sky Sports)***

### MSHAHARA WA MESSI KUFURU

KLABU yoyote itakayotaka kumsajili Messi itatakiwa kulipa kiasi cha pauni milioni 90 kwa mwaka kama mshahara wake ambao analipwa pale Barcelona. ***(Times)***

### BROOKS AWEKWA SOKONI

WINGA wa Bournemouth na timu ya Taifa ya Wales, David Brooks mwenye umri wa miaka 23, amewekwa sokoni na ni chaguo zuri kwa Manchester United kama hawataki kulipa pauni milioni 108 kwa Jadon Sancho. ***(Express)***

### YAKWAMA KWA BADIASHILE

OFA ya Manchester United ya pauni milioni 22 kwa mlinzi wa Ufaransa, Benoit Badiashile, mwenye umri wa miaka 19, imekataliwa na Monaco. ***(Star)***

### YAKARIBIA KWA DOHERTY

TOTTENHAM Hotspurs inakaribia kumsajili mlinzi wa kulia wa Wolverhampton Wanderers, Matt Doherty, 28. Wolves inataka kiasi cha pauni milioni 20 kwa ajili ya mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Ireland, lakini Spurs ina matumaini itapunguza. ***(Independent)***

### ALCANTARA KUSEPA BAYERN

THIAGO Alcantara, 29, anatarajia kuondoka kwa mabingwa wa Ulaya, Bayern Munich. Mabingwa hao wa Bundesliga, wanataka pauni milioni 30 na Liverpool imekuwa ikihusishwa kumwania kiungo huyo raia wa Hispania. ***(Express)***

### WEST BROM WAMTAKA EZE

KLABU ya West Brom iliyopanda daraja imewasiliana na Queens Park Rangers kwa ajili ya kumsajili winga wa Uingereza, Eberechi Eze, 22. ***(Birmingham Live)***

### BRIGHTON KUMBAKIZA WHITE

KLABU ya Brighton inaangalia uwezekano wa kumbakiza mlinzi wake, Ben White, 22, ambaye msimu uliopita alicheza kwa mkopo kule Leeds United, licha ya kupokea ofa kutoka Liverpool, Chelsea na Manchester United. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# Rashidi Juma kwa mkopo Polisi Tanzania

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Polisi Tanzania ambayo kwa muda mrefu ilikuwa kimya, imeibuka na kuanza usajili kwa kishindo, huku pia ikimchukua winga Rashid Juma (pichani) kwa mkopo wa mwaka mmoja kutoka Simba.

Kwa mujibu wa ukurasa rasmi wa mtandao wa kijamii wa klabu hiyo, ulimuonyesha mchezaji huyo akikabidhiwa jezi na mmoja wa viongozi wa klabu hiyo na kueleza furaha yao kumpa mchezaji huyo.

"Kwa furaha kubwa tunapenda kumtambulisha winga Rashid Juma kutoka Klabu ya Simba. Amekuja kwa mkopo wa mwaka mmoja, umoja wetu ndiyo nguvu yetu." Ilimaliza taarifa hiyo.

Mbali na mchezaji huyo, Polisi Tanzania pia imemsainisha mmoja wa mastraika hatari msimu wa Ligi Kuu uliomalizika, Daruweshi Saliboko akitokea Lipuli ya Iringa.

Straika huyo alimaliza Ligi Kuu akiwa na mabao tisa kwenye kikosi cha Lipuli ambacho kimeshuka daraja.

Pia imemsajili straika Ramadhani Kapora kutoka KMC, ambapo mtandao wa Polisi Tanzania umeandika kuwa ni mmoja wa wachezaji waliopendekezwa zaidi na benchi lao la ufundi ili kuongeza nguvu safu ya ushambuliaji.

Wachezaji wengine ni Kassim Haruna kutoka Sahare All Stars ya Tanga, na Datus Peter akitokea Mbao FC ambayo imeshuka daraja.

Polisi Tanzania ni moja kati ya timu zilizocheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu uliomalizika na kufanya vema, ikimaliza katika nafasi ya tano ikiwa na pointi 55.




# KAHATA AMFURAHIA MORRISON, WENZAKE

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA wengi kuamini kuwa nafasi yake ipo rehani baada ya Simba kumsajili Mghana Bernard Morrison, kiungo fundi wa timu hiyo, Mkenya Francis Kahata, amesema upana wa kikosi hicho cha mabingwa wa Ligi Kuu Bara utachangia ushindani wenye tija ndani ya timu.

Katika dirisha hili la usajili Simba imesajili nyota wapya saba, wazawa watatu, mabeki Ibrahimu Ame, David Kameta 'Duchu' na straika Charles Illamfya, huku wa kimataifa wakiwa wanne ambao ni beki Mkenya Joash Onyango, mshambuliaji Mkongomani Chris Mugalu, na viungo Mzambia Rally Bwalya na Morrison, ambaye anaonekana kutishia namba ya Kahata katika kikosi cha kwanza.

**Lakini Kahata amesema kikosi cha Simba kimesheheni wachezaji wengi wazuri ambao pia wanacheza timu za taifa wanapotoka, hivyo kwake anaona ni vizuri katika kuongeza ushindani wa namba.**

Kiungo huyo alisema upana wa kikosi msimu uliopita ulikuwa chachu ya kushinda mataji matatu, jambo ambalo litaongezeka zaidi msimu huu kutokana na kikosi kuimarishwa.

Msimu uliopita tulitwaa Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Bara na Kombe la FA.

"Simba ina kikosi kipana kilisheheni wachezaji wengi wazuri ambao pia wanachezea timu zao za taifa,"Kahata ambaye msimu uliopita alifunga mabao manne kwenye Ligi Kuu Bara ikiwemo pia kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa mwezi Desemba, aliiambia tovuti ya klabu hiyo.

Simba itashuka katika dimbani la Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Jumapili kuvaana na Namungo FC kwenye mechi ya Ngao ya Jamii ambayo ni maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara unaotarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu.

VIFAA...




Meneja Uhusiano wa SportPesa Tanzania, Sabrina Msuya (kulia) na Ofisa Mhamasishaji wa Klabu ya Yanga, Antonio Nugaz, wakikabidhi vifaa vya michezo kwa wawakilishi wa timu ya Kaptain Sports Centre ya Mbagala jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kuelekea kilele cha SportPesa Wiki ya Mwananchi. Makabidhiano hayo yalifanyika jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: SPORTPESA**

# *Sey, Salamba kupikwa kumrithi Lusajo*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thierry Hitimana, amesema anawaandaa nyota wake wawili, Mghana Stephen Sey na Adam Salamba kurithi nafasi ya mshambuliaji wao, Reliant Lusajo aliyejiunga na KMC FC akiwa mchezaji huru.

Akizungumnza na gazeti hili jijini jana, kocha huyo alisema baada ya kumkosa Lusajo, ambaye alikuwa katika mipango yake, sasa nafasi ya nyota huyo itachukuliwa na Sey akitokea Singida United na Salamba aliyewahi kuicheza Simba wakati huo akitokea Lipuli FC.

Alisema ana asilimia kubwa na Sey kuchukuwa nafasi ya Lusajo baada ya kuonyesha kiwango kizuri na katika mechi yao ya kirafiki iliyopita dhidi ya Azam FC, alifunga bao akiitendea vema krosi ya Shiza Kichuya.

"Hiyo mechi tulifungwa ila Sey alionyesha kiwango kizuri, lakini pia Salamba ni mmoja ya wachezaji ambao natarajia kuwatengeneza kuja kurithi nafasi ya Lusajo ambaye siko naye katika kikosi msimu huu," alisema Hitimana.

Alisema anaimani na uongozi wa timu hiyo kumalizana na Blaisa Bigirimana ambaye ataendelea kuimarisha safu hiyo ya ushambuliaji na kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita.

"Bigirimana na uongozi unaendelea kuzungumza kuongeza mkataba, lakini kuna Lucas Kikoti na Shiza Kichuya na wengine watakuwa msaada mkubwa kupata kile ambacho tunakitarajia," alisema Hitimana.

Kocha huyo, alisema kwa sasa wanaendelea na maandalizi ya msimu wa 2020/21 kuhakikisha wanafanya vizuri ila mawazo yake yapo katika mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Simba utakaopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

# Michezo

Ijumaa Agosti 28, 2020

Nipashe




‘Hayupo wa kumnunua Messi’ UKURASA 22

**NANI ZAIDI LEO?...**



Promota Jay Msangi akiwatambulisha Mabondia Dulla Mbabe (kulia) na Twaha Kiduku baada ya kupima uzito katika Uwanja wa Kinesi jijini Dar es Salaam jana. Mabondia hao watapanda ulingoni leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Yacouba apeperuka, Carlinhos atoa neno*

## ●●● Injinia Hersi awashangaa kwenda kumpokea, kiungo Muangola asema safari ya makombe...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa Yanga waliofika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana tayari kumpokea mshambuliaji raia wa Burkina Faso, Sogne Yacouba, wakiambulia ‘hewa’, kiungo Muangola Carlos Stenio Fernandes Guimaraes ‘Carlinhos’, ametoa neno la faraja kwao.

**Juzi Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alinukuliwa akiwataka mashabiki wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanja wa ndege kwa ajili ya kumpokea straika huyo aliyekuwa akiichezea Asante Kotoko ya Ghana msimu uliomalizika.**

Lakini mashabiki waliojitokeza kwa wingi uwanjani hapo, waliambulia hewa baada ya mchezaji huyo aliyetarajiwa kutua jana mchana kutotokea hadi saa 10:00 jioni. Hata hivyo, mashabiki hao waliojitokeza kwa wingi kwa ajili ya kumpokea Yacouba, waliondolewa na polisi walikuwapo katika uwanja huo, kwa kuelezwa kwamba hakuna taarifa zozote za mchezaji huyo kutua nchini jana.

Waandishi wetu walipomtafuta Bumbuli kujua kulikoni, mchezaji huyo hakutokea kama alivyonukuliwa juzi, simu yake iliita bila majibu.

Na Nipashe lilipomtafuta Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Mhandisi Hersi Saidi, wanaoidhamini Yanga, na ambao wamekuwa bize kushughulikia masuala yote ya usajili ya klabu hiyo katika dirisha hili, alisema anashangaa kusikia kuhusu taarifa za mchezaji huyo kuwasili nchini jana.

“Hakuna kitu kama hicho cha mchezaji huyo kuingia leo (jana),” alisema Hersi.

Katika hatua nyingine, mapokezi mazito aliyoyapata kiungo mpya wa Yanga, Carlinhos, kutoka kwa mashabiki wa klabu hiyo wakati akitua jijini Dar es Salaam Jumanne wiki hii, akitokea kwao Angola, yamekuwa deni kwake jambo ambalo amesema hiyo ni safari ya makombe imeanza.

Carlinhos anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, ambaye amejiunga na Yanga kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Klabu ya G.D. Interclube ya Angola, amesema kamwe hataiangusha klabu hiyo kutokana na namna mashabiki wake walivyoonyesha kumkubali.

“Nimeguswa sana na mapokezi makubwa na kukubalika mlikonionyesha wakati wa kuwasili kwangu, naahidi kamwe sitowaangusha, safari ya ubingwa na makombe mengi imeanza na mimi ni sehemu tu ya hayo, Mungu ibariki Yanga sc, Mungu bariki Soka la Tanzania,” aliandika Carlinhos katika mtandao wake wa kijamii.

Carlinhos ambaye amepewa jezi namba 11 iliyokuwa ikivaliwa na straika Mnyarwanda Patrick Sibomana msimu uliomalizika, tayari ameungana na wachezaji wengine wapya watatu katika mazoezi ya timu hiyo, ambao ni Mghana Michael Sarpong na Wakongomani wawili, Tuisila Kisinda pamoja na Mukoko Tunombe.

Ikiwa chini ya kocha Juma Mwambusi kwa sasa, mashabiki wa Yanga watapata fursa ya kushuhudia nyota hao wapya kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Aigle Noir Makamba FC ya Burundi katika mchezo wa kilele cha Wiki ya Mwananchi itakayopigwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam Jumapili.

# Miquissone, Wawa wainogesha Simba

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba, kiungo mshambuliaji Luis Miquissone na beki wa kati, Paschal Wawa wamerejea nchini baada ya kumaliza majukumu yao ya kifamilia katika mapumziko mafupi waliokuwa wameomba.

Wachezaji hao waliwasili jana mchana na kuungana moja kwa moja na wenzao ambao wako kambini kujiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii Jumapili dhidi ya Namungo FC pamoja na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Miquissone ambaye ni raia wa Msumbiji na Wawa kutoka Ivory Coast, hawakuwapo kwenye Tamasha la Simba Day lililofanyika Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam, na uongozi wa klabu hiyo ulieleza kuwa waliomba kurejea kwao kwenda kuoa.

Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa klabu hiyo ni kwamba Miquissone na Wawa, watakuwa sehemu ya kikosi kitakachoenda Arusha kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Namungo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha Jumapili.

Kuwasili kwa Miquissone kumepunguza minong’ono na wasiwasi kwa baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba ambapo walikuwa wakiteswa na tetesi kuwa hatorejea tena kwenye klabu hiyo kwa sababu amemaliza mkataba wake wa mkopo wa miezi sita kutoka Mamelodi Sundown ya Afrika Kusini.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042